# FAHAMU YA HIZB UT TAHRIR

Taqiuddin An-Nabahani

Hizb ut Tahrir

**<u>Chapa ya Uhariri wa 1440H / 2019M</u>**

**Fahamu ya Hizb ut Tahrir**

Tangu katikati mwa karne ya kumi na mbili hijriya (karne ya kumi na nane miladiya) ulimwengu wa Kiislamu una poromoka kutoka nafasi yake mporomoko ulio wa haraka, na ukazorota uzorotevu unaofedhehesha. Majaribio mbali mbali yaliyo jaribiwa kutaka kuuamsha au kuzuia kuendelea kuzorota lakini halikufaulu hata jaribio moja miongoni mwa majaribio hayo. Na ukabakia ulimwengu wa Kiislamu katika hali ya kukosa matumaini kwa fujo na kuzorota, mpaka sasa unahisi maumivu haya ya kubakia nyuma na mchafuko.

Amma sababu ya kuzorota kwake, hurudia kwa jambo moja nalo ni udhaifu mkubwa uliosibu akili katika kufahamu Uislamu. Na sababu ya udhaifu huu ni kutenganishwa nishati ya lugha ya Kiarabu na nishati ya Kiislamu pindi ilipopuuzwa lugha ya kiarabu katika kufahamu Uislamu na kuutekeleza tangu mwanzo wa karne ya saba hijriya. Ikiwa hakutaunganishwa nishati ya kiarabu na nishati ya Kiislamu kwa kuifanya lugha ya kiarabu—ambayo ni lugha ya Uislamu—sehemu muhimu isiyo tenganishwa nayo, utabakia uzorotevu ukiwazorotesha Waislamu kwa sababu nishati ya lugha ndiyo iliyobeba nishati ya Kiislamu na kuungana nayo kiasi ambacho haimkiniki kuutekeleza Uislamu utekelezaji ulio kamilika bila kwayo. Na kwa sababu ya kupuuzwa kwake itafanya ijtihadi (uvuaji wa hukumu) katika Shari'ah ikosekane, wala haimkiniki ijtihadi katika Shari'ah ila kwa lugha ya kiarabu kwa sababu lugha ya kiarabu ni sharti ya ki-msingi ya ijtihadi. Na ijtihadi ni dharura kwa Ummah kwa sababu Ummah hausongi mbele ila kwa kuwepo ijtihadi.

Amma sababu ya kushindwa kwa majaribio yaliyojaribiwa kuwainusha Waislamu kupitia Uislamu, huregea kwa mambo matatu.

- La kwanza ni kukosekana ufahamu sahihi juu ya fikra ya Kiislamu kwa upande wa waliobeba jukumu la muamko.
- La pili ni kukosekana uwazi wa twarika (njia) ya Kiislamu kwao katika kuitekeleza fikra yake.

- La tatu ni kutounganisha kwao fikra ya Kiislamu na twarika ya Kiislamu muungano barabara usioweza kutenganishwa.

Amma katika upande wa fikra ya Kiislamu, imesibiwa na mambo yaliyo ichafua, hali iliyo wafunga macho Waislamu wengi na usafi wake (usafi wa Uislamu). Na sababu za uchafu huu ulianza tangu mwanzo wa karne ya pili hijriya mpaka kuja kwa ubepari. Zilikuwa falsafa za kigeni kama za Kihindi, Kifursi, na Kiyunani (Kigiriki) zina athari kwa baadhi ya Waislamu iliyo wapelekea kujaribu kuunganisha baina ya Uislamu na falsafa hizi, licha ya kuweko mgongano kamili baina yake na Uislamu.  Majaribio hayo ya kuunganisha yalipelekea tafsiri na maelezo ya kimakosa ambayo yalitatiza na kuweka mbali baadhi ya hakika za Kiislamu katika mabongo ya Waislamu au kudhoofisha ufahamu wao wa Uislamu. Pamoja na hayo, ilikuwa kuingia kwa baadhi ya mahasidi wa Uislamu katika boma lake—kwa unafiki—na kutia katika Uislamu fahamu ambazo ziko mbali na Uisilamu bali ni zenye kugongana nayo. Hili lilipelekea katika kuufahamu Uislamu ufahamu uliochanganyikiwa kwa Waislamu wengi. Kisha ikaongezeka juu ya hayo katika karne ya saba hijriya, kupuuzwa lugha ya ya Kiarabu katika kuubeba Uislamu. Yakawa yote hayo ni sababu ya kuzorota Waislamu. Mwishoni mwa karne ya kumi na moja hijriya (karne ya kumi na saba miladiya) mpaka leo, ulimwengu wa Kiislamu umevamiwa kithaqafa na kimishenari na kufuatiwa na uvamizi wa kisiasa kutoka kwa Wamagharibi, na ikaongeza madhara juu ya madhara na kusababisha matatizo zaidi ndani ya mujtama wa Kiislamu. Yote hayo yalikuwa na athari ya kikweli juu ya Waislamu kufahamu makosa fikra ya Kiislamu mpaka ukapotea usafi wa kihakika katika mabongo ya Waislamu.

Amma twarika ya Kiislamu, hakika Waislamu walikosa ufahamu msafi juu yake. Waislamu walikuwa wakifahamu kuwa kuwepo kwao katika maisha ni kwa ajili ya Uislamu, na kuwa kazi ya Muislamu maishani ni kubeba ulinganizi wa Kiislamu na kazi ya serikali ya Kiislamu ni kutabikisha Uislamu na kutekeleza hukumu zake kindani na kubeba ulinganizi wake kiinje na njia ya hilo ni jihadi inayo tekelezwa na serikali. Twasema Waislamu, baada ya kujua hayo, walibadilika na wakaona kuwa kazi ya Muislamu mwanzo ni kuchuma dunia, kisha pili ulinganizi na kuongoza (kwa mujibu wa Uislamu) ikiwa dhurufu zitaruhusu. Na ikawa serikali haioni kosa au uzito (dhambi) wowote katika kulegea kwake katika kutekeleza hukumu za Kiislamu wala haikuona aibu yoyote katika kutopigana kwake jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu na kueneza Uislamu. Kisha Waislamu baada ya kuikosa serikali yao - licha ya udhaifu na upungufu wake wakaona Uislamu utarudi kwa kujenga miskiti, kutunga vitabu na malezi ya kiakhlaqi wakinyamazia ubwana wa ukafiri, na ukoloni wake, juu yao.

Amma katika upande wa kufungamanisha fikra na twarika Waislamu wamekuwa wakizisoma hukimu za kiShari'ah zinazo ambatana na utatuzi wa

matatizo - yaani zinazoambatana na fikra wala hawakushughulisha nafsi zao na hukumu ambazo hubainisha jinsi ya kutatua -yaani zile ambazo hubainisha twarika. Hivyo basi wakajishughulisha na hukumu zilizo tenganishwa na njia (*twarika*) ya kutekelezwa kwake. Wakajishughulisha na kusoma hukumu za swala, saumu, ndoa na talaqa na wakapuuza kusoma hukumu za jihadi, ngawira (*ghanaim*), hukumu za Khilafah, ukadhi, hukumu za kharaji na zinazo shabihiana nazo. Kwa hilo wakatenganisha fikra na twarika (*njia*) mpaka ikazaliwa kutokamana na hayo kutowezekana kutekeleza fikra bila twarika.

Na ikaongezwa juu ya hayo yote katika mwishoni mwa karne ya kumi na tatu hijriya (karne ya kumi na tisa miladiya) kosa katika kufahamu Shari'ah ya Kiislamu ili kuitabikisha juu ya mujtama likawa liko wazi. Ukawa Uislamu una fasiriwa tafsiri isiyo kubaliana na dalili (*nusus*) zake ili iwafikiane na mujtama uliopo, lakini la wajibu ni kuubadilisha mujtama ili uwafikiane na Uislamu sio kujaribu kufasiri Uislamu ili uwafikiane na mujtama. Kwa sababu suala hapa ni kuwa kuna mujtama ulio fisidika unaotakikanwa kurekebishwa na mfumo basi ni wajibu utabikishwe mfumo kama ulivyo na kubadilisha mujtama kwa jumla mbadiliko wa kimapinduzi juu ya msingi wa mfumo huu. Maana yake ni lazima kwa wanaojaribu kurekebisha kwamba watabikishe Uislamu kama ulivyokuja bila kuuangalia mujtama au zama au wakati au mahali. Lakini wao hawakufanya hivyo bali walifanya tafsir ya kimakosa juu ya hukumu za Kiislamu ili ziendane na zama hizi. Kuzidi kwa kosa hili kukadhihirika katika kuvua misingi jumla na fafanuzi. Wakavua (istinbat) qaida za kijumla na hukumu fafanuzi zinazo afikiana na mtazamo huo. Pindi walipoweka qaida tofauti tofauti za kijumla za kimakosa kwa mfano: (*Haikatazwi kubadilisha hukumu kwa kubadilika wakati*) na mfano: (*Ada ndio zinazo hukumu*) na nyenginezo. Wakafutu kwa ahkamu zisizokuwa na mategemeo katika Shari'ah bali wakafutu baadhi ya ahkamu zinazo gongana na dalili ya kukatikiwa ya Qur'ani. Kwa mfano: Wakahalalisha riba chache kwa kisingizio kwamba sio nyingi, na kwa hoja ya udharura kwa mali ya ambaye hajabaleghe (*qassir*), na akawa kadhi aliyeitwa (Kadhi wa Shari'ah) akihukumu na riba katika akiba ya mayatima kama yule kadhi aliyeitwa (Kadhi jumla) akihukumu na riba pia. Wakatoa fatwa kuwa kusitishwe kutumia Hudood (adhabu kwa mujibu wa vyanzo vya Uislamu) na wakaruhusu kutoa adhabu kutoka katika vyanzo ambavyo si vya Uislamu. Hivi ndivyo walivyoweka hukumu zinazo ikhtalifiana na Shari'ah kwa hoja ya kuwa zaafikiana zaidi na zama, na udharura wa kuafikiana na Shari'ah na kila zama, wakati na mahali; na natija ya hayo ni kuweka Uislamu mbali na maisha. Wakatumia maadui wa Uislamu, kupitia ufahamu huu ulio changanyikiwa na hukumu hizi za kibatili, kama chombo cha kuwaingizia Waislamu kanuni zao na mifumo yao bila ya Waislamu kuhisi mgongano wowote na dini yao, kwa sababu ya yale yaliyo kita katika fahamu zao, kwa ajili ya ufahamu ulio changanyikiwa kwamba Uislamu huafikiana na kila wakati na mahali. Kukawa *kufasiri kimakosa* Uislamu kwa ulimi wa wengi ili uafikiane na kila madhhab, mfumo, tukio na

msingi (*qaida*) hata kama tafsiri yao hukhitalifiana na mfumo wa Kiislamu na mtazamo wake. Hii ilichangia kuweka Uislamu mbali na maisha, kwa hivyo ilikuwa ni jambo la lazima kushindwa kwa kila harakati ya marekebisho inayopelekwa kwa mujibu wa ufahamu huu wa kigonjwa.

Katika mwanzo mwa karne ya ishirini miladiya ikaongezwa juu ya hilo, kilicho makinisha vizuizi vilivyosimama baina ya Uislamu na maisha, na kuzidisha juu ya taabu, juu ya taabu nyengine zilizosimama mbele ya harakati za Kiislamu. Na hili ni kuwa Waislamu, khasa wanavyuoni (*ulamaa*) na wasomi, kwa wakatu huu walisifika kwa mambo matatu:

**La kwanza** ni kuwa walikuwa wakiusoma Uislamu kwa njia inayo ikhtalifiana na njia ya kuusoma kwake katika kuufahamu. Ama njia ya kuusoma Uislamu ni kuzisoma hukumu za kiShari'ah kama mas’ala ya kivitendo ya kutabikishwa na serikali kwa yale yanayo husika nayo, na kwa upande wa kibinafsi kwa mambo yanayo husikana na yeye (*mtu binafsi*). Kwa hilo wanayvuoni waliifafanua *fiqhi* kwamba ni:

**علم با لمسائل الشرعية العملية المستنبطة من أدلتها التصفيلية**

***“Elimu (ujuzi) ya mas’ala ya kiShari'ah ya kivitendo yaliyo vuliwa kutokamana na dalili zenye maelezo mapana.”***

Kwa hilo huwa masomo haya yamezaa matunda ya kielimu kwa mwanafunzi, na kivitendo kwa mujtama katika serikali na kwa watu binafsi. Isipokuwa wajuzi (*maulamaa*) na wanafunzi hawa, na hata aghlabu ya Waislamu waliusoma Uislamu kwa mujarad ya elimu ya kinadharia kama kwamba ni falsafa ya kinadharia inayo wazwa. Kwa hivyo zikawa hukumu za kifiqhi ni za kimawazo si zenye kutendwa. Na ikawa Shari'ah ni yenye kusomwa kama ma’sala ya kiroho na kiakhlaqi na sio hukumu za kutatua matatizo maishani. Huu ni kwa upande wa kusoma.

Amma kwa upande wa kulingania Uislamu, ikawa imeathiriwa na njia za kimawaidha na uongofu unao fuatwa na wa mishinari sio kwa njia ya kufundisha inayo takikaniwa na Uislamu. Kwa haya wakawa wajuzi (*maulamaa*) katika Uislamu ni imma wanavyuoni waliolala kana kwamba wao ni vitabu vinavyozunguka au imma ni watoaji mawaidha na uongofu wanao wakariria watu maneno (*khutba*) matupu bila ya kuwa na athari yoyote katika mujtama. Wala hawakufahamu maana ya kulea na thaqafa ya Kiislamu ambayo humaanisha kuwafundisha Waislamu mambo ya dini yao mafundisho yanayo athiri hisia zao na kuwakhofisha na adhabu ya Mwenyezi Mungu na ghadhabu zake mpaka awe Muislamu ana nishati inayoathiri pindi inapounganishwa hisia zake na akili yake. Hayo ni kupitia kufundishwa kwa aya za Mwenyezi Mungu na kwa njia ya kufundishwa kwake (*Uislamu*). Hakika hawakufahamu hilo, wakabadilisha njia ya kufundisha inayoathiri

kindani, na wakaweka njia ya mawaidha na uongofu (*wa adh wa irshad*) ambayo hufungika katika maneno (*khutba*) matupu. Ikawa kupitia hayo waliona kuwa kuna mgongano baina ya kutatua matatizo ya mujtama na baina ya (*utatuzi wa*) Uisilamu unayohitaji muafaka. Hivyo basi ikawa ni jambo la kawaida kwa watu kufasiri Uislamu ili uafikiane na zama.

Na juu ya hilo, walifahamu vibaya kauli yake ta'ala:

**{ وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُوا كَافَّةً فَلَوْلاَ نَفَرَ مِنْ كُلِّ فِرْقَةٍ مِنْهُمْ طَائِفَةٌ لِيَتَفَقَّهُوا فِي الدِّينِ وَلِيُنْذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ }**

"***Wala haiwafalii Waislamu wote kutoka. Lakini kwa nini hawatoki baadhi katika kila kundi miongoni mwao, wakajifunze vyema Dini, na kisha kuwaonya wenzao watakapo warejea ili wapate kujihadharisha*.**"
[At-Taubah 9: 122].

Wakaifasiri Aya hii kumaanisha katika kila kikundi (*cha watu*) kutoke kipote kinacho jifundisha dini na kisha kurudi kuwafundisha watu wao. Kwa hivyo wakafanya kujifundisha dini ni faradhi ya kujitosheleza (*fardh kifaya*) na kwa hilo wakakhalifu Hukumu ya kiShari'ah kama walivyokhalifu maana ya Aya.

Amma hukumu ya kiShari'ah, nayo ni wajibu kwa kila Muislamu aliye baleghe na mwenye akili timamu ajifundishe katika dini mambo yanayo mlazimu maishani mwake. Hii ni kwa sababu yeye ni mwenye kuamrishwa kupeleka maisha yake yote kwa maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu. Na hakuna njia ya kufikia hilo ila kwa kujua hukumu za kiShari'ah zinazo ambatana na vitendo vyake. Hivyo basi huwa kujifundisha ilimu pana katika dini juu ya ahkamu zinazo mlazimu Muislamu maishani mwake ni fardhi ya kibinafsi (*fardh 'ayn*) sio fardhi kifaya. Amma ijtihadi nayo ni kuvua (*istinbat*) ahkamu, hino ni fardhi kifaya.

Amma kukhitalifiana kwao kwa maana ya Aya hii, hakika ya aya ni aya ya jihadi. Nayo humaanisha kuwa haijuzu kwa Waislamu wote kutoka katika jihadi; kitoke kikundi kwa ajili ya jihadi na libakie pote linalo jifundisha hukumu kwa Mtume (saw) mpaka wanaporegea mujahidina, hufundishwa na waliobakia yaliyowapita katika hukumu za Mwenyezi Mungu mafundisho yanayo athiri fahamu zao. Na pia dalili juu ya haya ni mifano kwa maswahaba (ra) katika umakini wao wa kujifundisha hukumu za dini na kujilazimisha kwao kwa Mtume (saw). Walikuwa baadhi yao wakitoka kwa vikosi vya jihadi na kubakia wanaobaki ili wajifundishe ahkamu za dini kisha wanaporudi mujahidina hufundishwa na waliobakia yale yaliyo wapita katika hukumu.

**Ya pili** ni kuwa mmagharibi hasidi anayechukia Uislamu na Waislamu aliiuhujumu dini ya Uislamu, akawa akiushambulia na kuuzulia na kwa upande mwengine hufanya zionekana kwa ubaya baadhi ya hukumu zake

pamoja na kuwa ndizo utatuzi sahihi za matatizo maishani. Wakawa Waislamu khasa walio wajuzi wanasifika na udhaifu mbele ya hujuma hizi. Hivyo basi wakauwacha Uislamu uwe ni wenye kutuhumiwa na wakawa wenye kuutetea mpaka kufanya majaribio ya kufasiri (*kimakosa*) hukumu za Kiislamu. Kwa mfano wakatafsiri jihadi kuwa ni vita vya kujitetea sio vita vya kushambulia. Kwa hilo wakakhalifu uhakika wa jihadi pamoja na kuwa jihadi ni vita na kila mwenye kusimama mbele ya ulinganizi wa Kiislamu sawa sawa awe ni mwenye kuonyesha uadui au la. Kwa lugha nyengine ni kuondoa kila kikwazo kinacho simama mbele ya da'wah ya Kiislamu yaani ulinganizi wa Uislamu na kupigana katika njia yake yaani katika njia ya Mwenyezi Mungu. Waislamu pindi walipopigana Jihadi dhidi ya Ufursi, Rumi, Masri, kaskazini mwa Afrika, Andalus na kwengineko hawaku shambulia ila kwa sababu ya ulinganizi unahitaji jihadi ili kuuneza katika biladi hizi. Kwa hivyo *tafsiri* hiyo juu ya jihadi ni kosa ambalo ni natija ya udhaifu wa kukubali Uislamu utuhumiwe na kutetewa kwake na utetezi unaodhihirisha kuwaridhisha wanaotuhumu. Na mfano wa haya ni suala la kuoa wake wengi, suala la kukata mkono wa mwizi na mengineo katika mas'ala ambayo Waislamu walijaribu kuwajibu makafiri. Wakawa wanajaribu *kutafsiri* Uislamu kwa mujibu wa *tafsiri* inayogongana nayo. Na ikawa natija ya kupitia yote hayo ni kuwekwa Waislamu mbali na kuufahamu Uislamu, na moja kwa moja kuwekwa Uislamu mbali na kutendwa kazi.

**Ya tatu** ni kwa sababu ilipokuwa serikali ya Kiislamu ikilika (ikisambaratika) kivuli chake (utawala wake) kutoka maeneo mengi ya Kiislamu na kunyenyekea kwake kwa hukumu za kikafiri, na kisha kuvunjika kwa serikali ya Kiislamu na kumalizwa kwake basi ikapatikana katika fahamu za Waislamu kutowezekana kuwepo kwa serikali ya Kiislamu na muhali wa kuhukumu kwa Uislamu peke yake. Kwa hivyo walikuwa wakiridhika kuhukumu kinyume na aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu. Wala hawakuona kosa katika hili maadamu imehifadhiwa jina la Uislamu hata kama hawahukumu nao. Na wakalingania uwajibu wa (kutumia) kustafidi na madhehebu na mifumo mengine ili zisaidie kwa utabikishaji wa Uislamu maishani. Natija ya haya ni kuwacha kazi ya kuregesha serikali ya Kiislamu na kunyamaza juu ya kutabikishwa hukumu za kikafiri juu ya Waislamu kwa mikono ya Waislamu.

Ikawa kwa sababu zilizo tangulia kuzoroteka harakati zote za mageuzi zilizo simama kuwapa Waislamu mwamko na kurudisha jaha ya Uislamu. Ikawa ni jambo la kawaida kuzoroteka kwake kwa sababu hata kama zilikuwa harakati za Kiislamu, lakini zilikuwa na ufahamu mbaya juu ya Uislamu lililozidisha tatizo na mushkila kuwa mgumu na kuuweka mujtama mbali na Uislamu badala ya kufanya kazi ili kuutabikisha juu yake.

Kwa haya ilikuwa hapana budi kuwa na harakati ya Kiislamu inayofahamu Uislamu, fikra na twarika, na kuunganishia baina yake na kufanya kazi ili

kurudisha maisha ya Kiislamu katika eneo miongoni mwa maeneo ya Kiislamu. Eneo hilo liwe ni nukta ya kuanzia (*nuqtat ibtidaa*) inayo chimbuka kutokana nayo ulinganizi wa Kiislamu kisha liwe ni nukta ya kusongea mbele (*nuqtat intilaq*) kwa ulinganizi wa Kiislamu.

Juu ya msingi huu, imebuniwa ***Hizb ut-Tahrir*** na ikasimama kufanya kazi ili kurudisha maisha ya Kiislamu katika biladi za kiarabu. Natija yake ya kutarajiwa kikawaida itakuwa ni kurudisha maisha ya Kiislamu katika ulimwengu wa Kiislamu kwa kuweko serikali ya Kiislamu katika eneo au maeneo kama nukta ya kusimamisha Uislamu, na kiini cha serikali kubwa ya Kiislamu, ambayo itarudisha maisha ya Kiislamu kwa kuutabikisha Uislamu na kubeba ulinganizi wa Kiislamu kwa ulimwengu wote.

Baada ya kusoma, fikra na uchunguzi, Hizb ut-Tahrir imetabanni hukumu za kiShari'ah, baadhi zinaambatana na utatuzi wa matatizo ya kibinafsi ambayo hutokea baina ya watu na katika mafungamano baina watu na watu wenzao mfano kuzuia kukodisha ardhi kwa ajili ya ukulima. Na miongoni yake ni yale yanayo ambatana na rai jumla iliyo dhihirika baina ya Waislamu jumla na wengineo (*wasiokuwa Waisilamu)* na nyenginezo (*rai*) zinazo husiana na mafungamano ya Waislamu na wengineo (*wasiokuwa Waisilamu*) mfano kuruhusiwa mikataba ya kidharura (*mu'ahudat idtirariyyah*) na ulinganizi kwa Uislamu kabla ya kuanza vita na yanayo shabihiyana na hayo. Na miongoni mwake ni yale yanayo ambatana na fikra nazo ni ahkamu za kisheria kama hukumu jumla kiShari'ah na hizo ni kama qaida za kijumla na istilahi zake (*ufafanuzi wa maana yake*). Kwa mfano:

**ما لا يتم الواجب إلا به فهو واجب**

**"*Kisicho timia wajibu ila kwayo basi hiyo ni wajibu*"**

Maana ya istilahi ya Hukm Shari'ah;

**خطاب الشارع المتعلق بأفعا العباد**

***"Ni khutuba ya Mtungaji Shari'ah kwa yanayo ambatana na vitendo vya waja"*** na mifano mengine ya istilahi.

Hakika Hizb imetabanni kanuni katika kila kitengo miongoni mwa hukumu, maalumu na ikawa inazilingania kila inapolingania Uislamu. Na hizi ni rai, fikra na hukumu za Kiislamu si nyengine na hazina ndani yake kitu chochote kisichokuwa cha Kiislamu wala haziathiriki na kitu chochote kisichokuwa cha Kiislamu bali ni za Kiislamu tu zisizo tegemea isipokuwa misingi na dalili za Kiislamu. Na Hizb inapotabanni ndani yake hutegemea fikra na huona kuwa ulinganizi wa Uislamu ni lazima msingi wake usimame juu ya fikra na ibebwe kama fikra kiongozi. Hii ni kwa sababu fikra ya kindani iliyo kamilika ndiyo inayosimama juu yake maisha na ndiyo inayo mwendeleza mwanadamu kwa msingi wake. Na ndiyo inayoonyesha uhakika wa vitu vikafamika ukwa ufahamu ulio sahihi. Na fikra haina budi ila iwe ya ***kindani*** ili iwe ***fikra ya***

***kindani iliyokamilika***. ***Fikra ya kindani*** ni mtazamo wa kindani juu ya vitu. ***Na fikra ya kindani iliyo kamilika*** ni mtazamo wa kindani juu ya vitu na hali zake na yanayo ambatana nayo na kustadili kwa hayo ili kufikia kwa natija ya kikweli. Na kwa maana nyengine ni mtazamo wa kindani uliokamilika juu ya vitu kwa hivyo hakuna budi ila kuwepo mtazamo wa kindani uliokamilika juu ya ulimwengu, uhai na mwanadamu na hakuna budi ila kuwepo mtazamo wa kindani uliokamilika juu ya mwanadamu na vitendo vya mwanadamu ili imkinike kufahamu hukumu zinazo fungamana juu yake.

Na mtazamo wa kindani juu ya ulimwengu, mwanadamu na uhai ndio unaotoa kutokamana nayo fikra jumla (*fikra kuliyya*) na ndio inayotatua tatizo kubwa kwa mwanadamu na ndiyo huwa ni *aqeeda*h (itikadi) kwa mwanadamu na ndiyo inayomuwekea mwanadamu lengo la maisha na lengo la vitendo anavyovitenda maishani. Kwa sababu mwanadamu huishi ulimwenguni na ikiwa halijatatuka tatizo kubwa katika nafsi yake na juu ya uhai anayoishi ndani yake na juu ya ulimwengu ambayo ni mahala pa maisha yake na kuwepo kwake haimkiniki kujua suluki (*tabia*) ambazo yampasa azifuate. Kwa hivyo imekuwa aqeeda (itikadi) ndiyo msingi wa kila kitu.

Na mtazamo wa kindani uliokamilika juu ya ulimwengu, mwanadamu na uhai hufikisha kwa aqeeda (itikadi) ya Kiislamu. Inayodhihirisha kwa uwazi kuwa hivyo ni viumbe vilivyo umbwa na Muumba na kuwa Muumba huyu ndiye peke yake anavyoviendesha na husimama kwa kuzihifadhi na kuziendesha kwa nidhamu makhsusi. Na kuwa maisha haya ya dunia sio ya kudumu wala si ya milele. Hupatikana aliyoko kabla ya maisha naye ni Muumba wake na mwendeshaji wake na hupatikana kilicho baada yake (baada ya maisha) nayo ni Siku ya Qiyama na kuwa vitendo vya mwanadamu katika maisha haya ya dunia ni lazima ya pelekwe kwa mujibu ya maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu. Na kuwa mwanadamu atahisabiwa juu yake Siku ya Qiyama nayo ni Siku ya Hisabu. Kwa hivyo huwa ni lazima kwa mwanadamu kujifunga na Shari'ah ya Mwenyezi Mungu ambayo imefikishwa kwake na Mtume Muhammad (saw).

Na mtazamo wa kindani uliokamilika juu ya ulimwengu, uhai na mwanadamu huonyesha kuwa vyote ni mada tu sio roho wala haikuundwa kutokamana na mada na roho. Maana ya mada hapa ni kitu kinacho hisika na kufahamika, sawa sawa ijulikane mada kama chenye umbo na uzito au ijulikane kama nishati ya kidhahiri au iliyofichika. Uchunguzi hapa si juu ya ni nini mada bali uchunguzi ni juu ya ulimwengu, uhai na mwanadamu—hivi vitu vinavyo hisika na kufahamika—kwa upande wa kuwa vimeumbwa na Muumba. Na maana ya roho hapa ni kudiriki fungamano na Mwenyezi Mungu sio maana ya siri ya uhai. Uchunguzi si juu ya roho kwa maana ya siri ya uhai bali uchunguzi ni juu ya fungamano la ulimwengu, uhai na mwanadamu kwa aliye ghaibu naye yaani Muumba na juu ya kudiriki fungamano hili. Kwa maana nyengine ni

kudiriki fungamano la ulimwengu, uhai na mwanadamu kwa Muumba wake, ni sehemu yake au si sehemu yake.

Mtazamo wa kindani uliokamilika juu ya ulimwengu, uhai na mwanadamu, kutoka upande wa maana ya roho kuwa ni kufahamu fungamano na Mwenyezi Mungu si upande wa roho kama siri ya uhai, huonyesha kuwa ni mada tu sio roho wala haikuundwa kutokamana na mada na roho. Amma kuwa ni mada ni kuwa viko wazi (vyaonekana) bila kufichika kwa sababu hudirikiwa na huhisiwa. Amma kuwa si roho hilo ni kuwa roho ni mwanadamu kudiriki fungamano lake na Mwenyezi Mungu (swt). Kudiriki hivi mwanadamu fungamano lake na Allah, si ulimwengu, mwanadamu wala uhai bali ni kitu chengine yasiyokuwa hayo. Amma kuhusu kuwa haikuundwa kutokamana na mada na roho, hilo ni wazi katika ulimwengu na uhai. Amma katika mwanadamu, hakika kudiriki kwake kwa fungamano na Mwenyezi Mungu si sehemu ya umbile/muundo bali ni sifa ya ziada kwa dalili ya kuwa kafiri anaye kanusha kuwepo Mwenyezi Mungu hadiriki fungamano lake na Mwenyezi Mungu na pamoja na hilo ni mwanadamu.

Na kwa haya, hakika yale wanayo yasema baadhi ya watu ya kuwa mwanadamu ameundwa kutokamana na mada na roho, na inaposhinda ndani yake mada juu ya roho huwa ni muovu na inaposhinda ndani yake roho juu ya mada huwa ni mwema na ni jukumu lake kufanya roho ishinde juu ya mada ili awe ni mwema. Msemo huu sio sahihi. Mwanadamu hakuundwa juu ya mada na roho na hilo ni kwa sababu roho inayochunguzwa katika mlango huu katika watu wote wanao amini kuwepo Muumba ni athari ya Muumba au kinacho shuhudiwa miongoni mwa athari katika upande wa yaliyofichika au kuwa kitu kinachodirikiwa ndani yake kuwa hakikupatikana ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu yaani kwa maana ya uroho au upande wa kiroho. Na roho kwa maana ya uroho au upande wa kiroho inayopatikana kwa mwanadamu sio siri ya uhai wala haitokamani na srii ya uhai wala haina mafungamano ya siri ya uhai, bali ni kitu chengine tofauti kwa dalili kuwa hayawani ana siri ya uhai na pamoja na hilo hana uroho wala upande wa kiroho wala hakuna yeyote anayesema kuwa yeye (hayawani) ameundwa juu ya mada na roho. Hali hii yaleta yakini kuwa roho kwa maana hii sio siri ya uhai wala haitokamani na siri ya uhai wala haina mafungamano na siri ya uhai. Kama alivyokuwa hayawani hakuundwa juu ya mada na roho pamoja na kuwa ana siri ya uhai, hivyo hivyo mwanadamu hakuundwa juu ya mada na roho hata kama anayo ndani yake siri ya uhai. Kwa sababu roho inayomtofautisha mwanadamu na inayopatikana kwake haifungamani na siri ya uhai wala haitokamani nayo bali ni kudiriki fungamano na Mwenyezi Mungu, basi haisemwi kuwa ni sehemu ya muundo ya mwanadamu kwa hoja ya kuwa ana siri ya uhai.

Na madamu roho inayochunguzwa hapa katika mlango huu ni kudiriki fungamano na Mwenyezi Mungu wala haina fungamano na siri ya uhai. Kwa

hivyo haiwi ni sehemu ya muundo wa mwanadamu kwa sababu kudiriki fungamano sio sehemu ya muundo wake bali ni sifa ya kiinje kwa dalili ya kuwa kafiri anaye kanusha kuwepo Mwenyezi Mungu hadiriki fungamano lake na Mwenyezi Mungu na pamoja na hilo yeye ni mwanadamu.

Pamoja na kuwa ulimwengu, mwanadamu na uhai ni mada wala sio roho lakini upande wake wa kiroho ni kuwa ni viumbe vilivyo umbwa na muumba na maana hiyo ndiyo fungamano lao, kwa sifa zao kama viumbe, na Mwenyezi Mungu (swt) ni muumba wao. Ulimwengu ni mada na hali yake kama kiumbe kilicho umbwa na muumba ndiyo upande wa kiroho ambao hudiriki mwanadamu. Na uhai ni mada na hali yake kama kiumbe kilicho umbwa na muumba ndio upande wa kiroho ambao hudiriki mwanadamu. Upande wa kiroho hautokamani na dhati ya ulimwengu au uhai au mwanadamu bali ni hali ya kuwa ni viumbe vilivyo umbwa na aliyeviumba ni Mwenyezi Mungu (swt). Fungamano hili ndilo upande wa kiroho.

Na asili katika maana ya roho ni kuwa watu ambao huamini kuwepo Mungu hurudia matamko ya roho, uroho na upande wa kiroho na hukusudiwa kutokamana nayo athari ya Muumba katika mahali au kinacho shuhudiwa katika upande wa *ghaibu* au hali ya kudirikiwa katika kitu kisichotokea ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Maana hizi huitwa kwayo roho, upande wa kiroho na uroho au kwa yale yenye maana sawa na hizi, maana jumla zisizoeleweka na zisizokuwa wazi. Hizi zina hakika ndani ya fahamu zao na zina hakika nje ya fahamu zao nayo ni *ghaibu* inayodirikiwa kuwepo kwake na isiyodirikiwa dhati yake na athari ya hii *ghaibu* katika vitu. Lakini uhakika huu ambao wanaouhisi hutokea kivitendo katika hisia zao lakini wao hawawezi kuifafanua (kuijua) kwa sababu si wazi kwao wao. Ikawa kwa sababu ya kutokuwa wazi maana hizi kwao ufahamu wao kwa maana hizi ukachanganyikiwa. Basi wakachangayikiwa kwa baadhi yao kufahamu kuwa roho ni siri ya uhai. Wakawa wanasema mwanadamu kuwa ameundwa kutokamana na mada na roho kwa sababu ya kuhisi kwao kuwepo roho ambayo ni siri ya uhai na kuwepo roho kwa maana ya uroho au upande wa kiroho. Wakadhania kuwa roho ndiyo ile (siri ya uhai) au kuwa zimetokamana na nayo na wala hawakumtazama hayawani aliye na roho yaani siri ya uhai wala hana uroho au upande wa kiroho. Na pia ilikuwa kutokamana na kutokuwa wazi kwao wakaanza kuita kila kinacho patikana kutoka kwa mwanadamu katika msukumo wa kibinafsi kuwa ni uroho; husema mtu juu ya nafsi yake kuwa anahisi uroho wa hali ya juu au fulani ana uroho mkubwa. Na ikawa pia kutokamana na kutokuwa wazi kwao wakawa wakenda mahali na kuhisi hapo utulivu au msisimko kisha husema mahala hapa kuna upande wa kiroho au uroho. Na ikawa pia kutokamana na kutokuwa wazi kwao akawa mtu akijiweka na njaa nafsi yake, kuutesa mwili wake na kuukondesha mwili wake akidai kuwa yeye anataka kuitia nguvu roho yake. Yote hayo ni kwa sababu ya kutokuwa wazi kwao maana ya roho, maana ya uroho na maana

ya upande wa kiroho. Mkanganyiko kama huo ulitokea hapo awali pale ambapo watu walijaribu kufahamu waqiah wa nini akili au kufikiri. Hakika akili ni tamko linalokusudiwa kutokamana nalo utambuzi/udirikaji na hukumu/uamuzi juu ya kitu na yaliyomo katika maana hii. Lakini waliotangulia walikuwa wakiona kuwa vitu hivi miongoni mwa utambuzi na nyengine ni athari ya akili sio akili yenyewe. Na kwao wao akili ni hakika wanayo ihisi lakini hawajabainikiwa uhakika wake nayo si wazi kwao. Na kwa sababu ya kutokuwa wazi kwao wao, ulikhtalifiana mtazamo wao kwake na kugongana mtazamo wao juu ya mahala pake na wakachanganyikiwa zaidi katika kudiriki kwake uhakika wake. Miongoni mwao wanasema iko katika moyo na miongoni mwao wanasema kuwa iko katika kichwa na miongoni mwao wapo wanaosema kuwa iko katika ubongo na wapo miongoni mwao wanaosema mengineyo. Na zilipokuja zama hizi, wakajaribu baadhi ya mufakirina kuweka wazi maana ya akili na kuifafanua; wakachanganyikiwa kwa kukosa kudiriki uhakika wake. Wakasema baadhi yao kuwa ni athari ya ubongo juu ya mada na wakasema wengineo kuwa ni athari ya mada juu ya ubongo. Mpaka mwishowe ilitambulikana utambuzi sahihi kuwa “akili” ni kunukuliwa uhakika (*waqi’ah*) mpaka katika ubongo kupitia hisia na maalumuti zilizotangulia zinazofasiri uhakika huo. Na kwa utambuzi huu ilidirikiwa ni nini akili. Na hivyo hivyo hakuna budi kwa baadhi ya mufakirina ila kufafanua uwazi wa maana ya roho, uroho na upande wa kiroho na yaliyomo katika maana ya haya, uwazi inayofanya fahamu kuzidiriki na kudiriki uhakika wake. Hii ni kwa sababu kuna uhakika wa roho, uroho na upande wa kiroho. Kwa sababu kinacho shuhudiwa na kuhisiwa na mwanadamu ni kwamba kuna vitu vya kimada anavyo vihisi mwanadamu na huenda akavishika kama mkate, na huenda kuvihisi wala asiweze kuvishika kama huduma za tabibu. Na kuna vitu vya ki-*ma’nawiya* (tabia) anavyo vihisi wala hawezi kuvishika kama ufahari na sifa. Na kuna vitu vya kiroho anavyo vihisi wala hawezi kuvishika kama kumcha Mwenyezi Mungu na kusalimu amri kwake wakati wa shida. Maana hizi tatu (roho, uroho na upande wa kiroho) zina uhakika anao uhisi mwanadamu na kutofautika moja wapo kutoka nyenginezo. Hivyo basi roho au upande wa kiroho au uroho ni hakika maalumu inayotokea hisia juu yake. Hapana budi ili kuzitambua hakika hizi ili kuziweka wazi kwa watu kama ilivyo tambulika akili na kuwekwa wazi kwa watu.

Uchunguzi katika hakika ya roho, uroho na upande wa kiroho hubainisha kuwa hazipatikani kwa (*mulhid*) mwenye kukanusha kuwepo Mwenyezi Mungu na kuwa hupatikana tu kwa wanaoamini katika kuwepo mola. Na hii humaanisha kuwa imefungamana kwa imani juu ya Mwenyezi Mungu, hupatikana mahala panapo patikana imani hii na huadimika inapo adimika. Na imani ya kuwepo Mwenyezi Mungu maana yake ni kusadikisha kuliko katikiwa kuwa vitu ni viumbe vilivyo umbwa na Muumba. Na huwa maudhui ya uchunguzi ni kuwa vitu ni viumbe vya Muumba. Kukiri kuwa vimeumbwa na Muumba ni imani, na kukanusha kuwa vimeumbwa na Muumba ni ukafiri.

Katika hali ya kukiri na kusadikisha kuliko katikiwa hupatikana upande wa kiroho, ambako kumetokana na kuamini. Na katika hali ya kukosekana kukiri na kukanusha haupatikani upande wa kiroho, ambako kumetokana na kukosekana kuamini. Basi huwa upande wa kiroho ni kule kuwa vitu vimeumbwa na Muumba yaani ni fungamano la vitu na Muumba wao kwa upande wa kuumbwa na kuundwa kutoka hali ya kutokuwepo. Fungamano hili, yaani kuwa vimeumbwa na Muumba, inapodirikiwa na akili hupatikana kupitia kudiriki huko hisia kwa ukubwa wa Muumba na hisia ya kumcha yeye na hisia ya kumtukuza; huwa kudiriki huku ndio inayozalisha hisia kwa fungamano hili nayo ni roho. Basi huwa roho ni kudiriki fungamano na Mwenyezi Mungu. Na kwa hayo huwa wazi maana ya upande wa kiroho na maana ya roho, nayo sio matamko yaliyo na maana ya kilugha ambayo huregelea maana yake kutokamana na lugha wala sio istilahi ambayo kila watu wawe na istilahi zao kama wanavyotaka wao. Bali ni maana zilizo na uhakika maalum vyovyote zitakavyo bandikwa majina. Uchunguzi huwa ni juu ya uhakika na maana hizi sio maana ya tamko la kilugha; uhakika wa maana hizi ni huu nayo ni kuwa roho inayolingana na upande wa kiroho katika mwanadamu ni kudiriki fungamano na Mwenyezi Mungu. Na upande wa kiroho katika ulimwengu, mwanadamu na uhai ni kule kuwa ni viumbe vilivyoumbwa na Muumba. Vyovyote litakavyo bandikwa tamko hilo huwa makusudio yake ni kwa maana hii kwa sababu ndiyo uhakika unaohisika na iliyosimama dalili ya kukatikiwa juu yake. Na kwa kuwa uhakika huu unaohisiwa ndio uhakika wa kindani na wa kinje kwa mtu anayeamini kuwepo Mola yaani kuwepo Muumba wa vitu.

Amma roho ambayo ni siri ya uhai nayo kuwepo kwake hakuna shaka na imethubutu kwa dalili za kukatikiwa za Qur'ani, na imani juu ya kuwepo kwake ni jambo la lazima nayo sio maudhui ya uchunguzi huu.

Na tamko la roho (*ruh*) ni tamko lililobeba maana nyingi kama *'ayn* inayobeba maana nyingi. Kama ilivyokuwa *'ayn* ni jina liitwalo vitu vyingi kama kuitwa mto (vyanzo vya maji), jicho, jasusi, dhahabu, fedha na mengineo. Hivyo hivyo *ruh* iko na maana nyingi. Imethubutu katika Qur'ani *ruh* kuwa na maana nyingi. Imekuja *ruh* kwa maana ya siri ya uhai:

**{ وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ قُلِ الرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّي وَمَا أُوتِيتُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِلاَّ قَلِيلاً }**

**"*Na wanakuuliza khabari za Roho. Sema: Roho ni katika mambo ya Mola wangu Mlezi. Nanyi hamkupewa katika elimu ila kidogo* tu"** [Al-Isra' 17:85]

Na imekuja kwa maana ya Jibril (as):

**{ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الأَمِينُ - عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنْ الْمُنذِرِينَ }**

**"*Ameuteremsha Roho muaminifu. Juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji*."** [Ash-Shu'ara 26: 193-194].

Na imekuja kwa maana ya Shari'ah ya Mwenyezi Mungu:

{ وَكَذَٰلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِنْ أَمْرِنَا }

**"*Na namna hivi tumekufunulia wahyi roho (Qur'ani) kwa amri tetu*"**

[Ash-Shura 42: 52]

Na maana haya yote sio yanayokusudiwa katika msemo huu wa upande wa kiroho au kitu cha kiroho au kutenganisha mada na roho au yanayo fanana nayo. Wala hakuna mahusiano katika kauli juu ya roho na maana ya roho yaliyothubutu katika Qur'ani bali maana iliyokusudiwa juu ya roho katika matamshi haya ya mwisho ni maana iliyofungamana na kuumbwa mada yaani kwa upande wa kuwa vitu vimeumbwa na Muumba naye ni Shari'ah ya Mwenyezi Mungu (swt) na kudiriki kwa mwanadamu fungamano la vitu kwa Muumba wake.

Na mtazamo wa ndani uliokamilika juu ya mwanadamu huonyesha kuwa yeye anaishi katika mizunguko miwili: **wa kwanza** ni ule unaomtawala yeye na **wa pili** ni ule anaoutawala yeye. Amma mzunguko ambao unaomtawala yeye ni mzunguko ambao ndani yake unatabikishwa nidhamu za kiulimwengu basi yeye hupelekwa pamoja na ulimwengu na uhai kwa mujibu wa nidhamu maalum isiyobadilika. Kwa hivyo hutokea vitendo juu yake katika mzunguko huu bila ya matakwa yake, na yeye huishi ndani yake bila kukhiyarishwa. Hakika yeye ameletwa katika dunia hii bila ya matakwa yake na ataiondoka bila ya matakwa yake, na yeye hamiliki uweza wa kutoka kwenye nidhamu ya kiulimwengu. Na kwa hivyo hataulizwa juu ya vitendo vinavyotokamana na yeye na juu yake katika mzunguko huu. Amma mzunguko ambao huutawala yeye nao ni mzunguko ambao yeye huenda ndani yake kwa khiyari kwa mujibu ya nidhamu anayoichagua sawa sawa iwe Shari'ah ya Shari'ah ya Mwenyezi Mungu au nyengineo. Katika mzunguko huu, hutokea ndani yake vitendo ambavyo hutokamana na mwanadamu au (*hutokea vitendo*) juu yake kwa matakwa yake. Yeye hutembea, hula, hunywa na husafiri katika wakati wowote autakao na hujizuia na hayo wakati wowote autakao. Hutenda kwa khiyari na hujizuia kwa khiyari kwa hivyo ataulizwa juu ya vitendo anavyo vitenda katika mzunguko huu.

Naye mwanadamu hupenda vitu vinavyo tokamana na yeye au juu yake katika mzunguko unaomtawala yeye na anaoutawala yeye, na huchukia vitu katika mizunguko hiyo. Na hujaribu kufasiri mapenzi haya na chuki hizi kuwa *kheri* na *shari*. Na huelekea kuita kila anacho kipenda kuwa ni *kheri* na anacho kichukia kuwa ni *shari*. Hivyo hivyo huviita vitendo kuwa ni *kheir* na vitendo vyengine kuwa ni *shari* kwa msingi wa kufikiwa kwake manufaa kutokamana navyo au kupatwa na madhara kutokamana navyo.

La uhakika ni kuwa vitendo ambavyo hutokea kutoka kwa mwanadamu katika mzunguko wake haijulishi kwa dhati yake kuwa ni *kheri* au *shari* kwa sababu

hivyo ni vitendo tu mujarad visivyo na sifa yoyote kwa dhati yake kuonyesha kuwa ni *kheir* au *shari*. Bali huwa *kheri* au *shari* tu kwa msingi wa hisabu ya kinje juu ya dhati ya vitendo. Hivyo kuuwa nafsi ya mwanadamu haiitwi *kheri* au *shari* bali huitwa tu mauaji. Kuwa kheri au shari huja tu kwa sifa nje yake inayokuja juu yake. Kwa hivyo huwa kumuua adui mpiganaji ni *kheri* na kumuua raia au aliye na ahadi (*mu'ahid*) au aliyepewa amani (*musta'man*) ni *shari*. Hulipwa (*thawabu*) muuwaji wa kwanza na huadhibiwa muuwaji wa pili pamoja na kuwa kitendo chao ni kimoja bila tofauti yoyote. *Kheri* na *shari* hutokamana na sababu zinazompelekea mwanadamu kutenda kitendo na lengo analolilenga katika kutenda kitendo hicho. Sababu zinazompelekea mwanadamu kutenda kitendo na lengo analolilenga ndani yake ndizo sababu mbili zinazoweka sifa za kitendo kuwa ni *kheri* na *shari* sawa sawa amependezwa mwanadamu au kuchukuzwa na sawa sawa amepata manufaa au madhara.

Na kwa haya imekuwa lazima kuchunguzwa sababu/dhurufu zinazompeleka mwanadamu kutenda kitendo na kuchunguzwa lengo ambalo hulilenga na wakati huo itafahamika ufahamu wa sawa lini kitendo husifiwa kuwa ni *kheri* au *shari*. Na ufahamu wa dhurufu zinazompeleka (*kutenda*) na lengo analolilenga (*katika kitendo*) hutegemea aina ya *aqeeda (itikadi)* anayoiamini mwanadamu. Basi Muislamu ambaye anamuamini Mwenyezi Mungu na kuamini kuwa Yeye ndiye aliyemtuma bwana Muhammad (saw) na Shari'ah ya Kiislamu inayobainisha maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo Yake, na kupanga mahusiano yake na Mola wake na nafsi yake na watu wengineo: **Ni lazima Muislamu huyu kupeleka mambo yake kwa mujibu ya maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu, na liwe lengo analolilenga katika mambo yake ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu**. Kwa hivyo huwa kitendo husifiwa kuwa cha kumghadhabisha Allah au kumridhisha; ikiwa ni chenye kumghadhibisha Mwenyezi Mungu kwa **kukhtalifiana** na maamrisho Yake na kuvunja makatazo Yake huwa ni *shari*, na ikiwa ni yenye kumridhisha Allah kwa **kutii** maamrisho Yake na kuepukana na makatazo Yake huwa ni *kheri*.

Kwa hayo twaweza kusema: *Kheri* kwa mtazamo wa Muislamu ni kila kinachomridhisha Mwenyezi Mungu na *shari* ni kila kinachomghadhabisha Mwenyezi Mungu.

Na haya hulingana na vitendo vinavyo tokamana na mwanadamu au juu yake katika mzunguko anaoutawala.

Amma vitendo vinavyo tokamana na mwanadamu au humtokea juu yake katika mzunguko unaomtawala yeye, mwanadamu huzisifu na *kheri* au *shari* kufuata **mapenzi** yake au **kuchukia** kwake au **kunufaika** kwake au **kudhurika** kwake:

**{ إِنَّ الإِنسَانَ خُلِقَ هَلُوعًا - إِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ جَزُوعًا- وَإِذَا مَسَّهُ الْخَيْرُ مَنُوعًا }**

***“Hakika mtu ameumbwa na papara (pasina subra). Inapo mgusa shari hupapatika (mwenye fazaa na wasiwasi). Na inapo mgusa kheri huizuilia”***

[Al-Ma'arij 70: 19-21]

Na:

**{ وَإِنَّهُ لِحُبِّ الْخَيْرِ لَشَدِيدٌ }**

**“*Naye hakika bila ya shaka ana nguvu za kupenda mali*.”**

[Al-'Adiyat 100: 8].

Ijapokuwa sifa hii haimaanishi sifa ya uhakika, kwa sababu huenda mwanadamu akaona jambo kuwa *kheri* kumbe ni *shari* na huenda akaona jambo kuwa ni *shari* kumbe ni *kheri*

**{ وَعَسَى أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ وَعَسَى أَنْ تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ }**

***"Lakin huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mpende kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua, lakini ninyi hamjui."***

[Al-Baqarah 2: 216]

Mtazamo wa kindani uliokamilika juu ya vitendo vya mwanadamu huonyesha kuwa ni mada tu kwa asili ya dhati yake ikivuliwa dhurufu na mazingatio yote. Na hali yake kama mada kwa dhati yake haijulishi kama ni zuri (*hasan*) au baya (*qabeeh*) bali hujulikana kwa hayo kutokamana na dhurufu zake za kinje na kwa mazingatio yanayo tokamana nayo na mengineo. Dhurufu hizi za kinje ambazo hubainisha kitendo kuwa ni kizuri au kibaya imma iwe ni **akili** pekee au **Shari'ah** peke yake; au imma iwe ni **akili na dalili yake iwe ni Shari'ah** au **Shari'ah na dalili yake iwe ni akili**. Amma kusifu kwa upande wa akili pekee, hino ni batili kwa sababu akili inasibiwa na udhaifu, kutofautiana, ikhtilafu na migongano. Basi vipimo vya akili kwa zuri (*hasan*) na baya (*qabeeh*) huathiriwa na mazingira anaoishi ndani yake bali hutofautika na kukhtalifiana kwa zama zinapobadilika. Na inapowachwa kipimo cha baya na zuri kwa akili huwa kitu ni kibaya kwa baadhi wa watu na kizuri kwa wengine, bali huenda kikawa kitu kimoja kuwa ni kizuri katika zama (fulani) na kibaya katika zama zengine. Uislamu kwa sifa yake kama mfumo wa kiulimwengu unaodumu milele hulazimu kuwa sifa ya kitendo kuwa kizuri au kibaya ni sawa sawa kwa wanadamu wote katika zama zote. Kwa hivyo hapana budi ila kubainishwa kitendo kuwa kizuri au kibaya kutokamana na nguvu iliyo juu ya akili ikawa hapana budi ili itokamane na Shari'ah. Kwa hivyo hino sifa ya kitendo cha mwanadamu kuwa kibaya au kizuri hutokamana na Shari'ah na kufikia hapa imekuwa udanganyifu ni uovu (*qabeeh)* na utekelezaji ahadi ni uzuri (*hassan)*, na ikawa ufasiki ni uovu (*qabeeh*) na uchaji mungu ni uzuri

(*hasan*), na ikawa uasi dhidi ya serikali ya Kiislamu ni uovu (*qabeeh*) na kuisahihisha (serikali) utekelezaji wake ikiteleza ni kitendo kizuri (*hasan*) kwa sababu Shari'ah ishabainisha hayo. Amma kufanya dalili ya Shari'ah kwa yaliyodokezewa na akili, hino hulazimisha kufanya akili ni yenye kuhukumu katika zuri na baya na tumekwisha bainisha ubatili wake. Amma kuifanya akili ni dalili kwa yaliyodokezwa na Shari'ah, hino hulazimu kuifanya akili ni dalili juu ya hukumu ya kiShari'ah. Lakini dalili ya hukumu ya kiShari'ah ni *nassi* (msemo wazi wa kiwahyi) sio akili, na jukumu la akili ni kufahamu hukumu ya kiShari'ah sio kuifanya dalili juu yake. Na kufikia hapa huwa zuri (*hasan*) na baya (*qabeeh*) ni kutokamana na Shari'ah tu sio akili.

Tofauti baina ya kusifu kitendo kuwa ni kheri (*khayr*) au shari (*sharr*) na baina kukisifu kuwa ni kizuri (*hasan*) au kibaya (*qabeeh*) ni kuwa kuisifu kuwa ni kheri na shari huwa kwa sababu ya athari yake katika mtazamo wa mwanadamu na kwa sababu ya kukitekeleza au kukipa nyongo (kukiwacha). Mwanadamu huita kila kinachomdhuru au kukichukia miongoni mwa vitendo kuwa ni shari, na huita kila kinacho mnufaisha na anachokipenda miongoni mwa vitendo kuwa ni kheri kwa sababu ya athari yake juu ya hilo bila kujua uzuri na ubaya hilo halipatikani kwake katika hali hili. Na kujengea juu ya mtazamo huu kukitekeleza kitendo au kukipa nyongo (kukiwacha). Ikaja usahihishaji kwa mtazamo huu kuwa kitendo hakisemwi kuwa ni kheri au shari kwa mujibu wa kuchukiwa na kupendwa au manufaa na madhara, bali kipimo cha kuwa kheri au shari ni **kumridhisha Mwenyezi** au **kumghadhabisha Mwenyezi Mungu (swt)**. Huu ndio uchunguzi wa upande wa kipimo cha kheri na shari ambacho watu wamekitambua na sio kwa upande wa kitendo chenyewe.

Amma kusifu vitendo kuwa ni vizuri au vibaya, hii ni katika upande wa hukumu juu yake kutoka kwa mwanadamu na kwa upande wa adhabu na thawabu. Hakika mwanadamu amejipa nafsi yake jukumu la kuhukumu kitendo kuwa ni kizuri au kibaya kama kipimo cha vitu. Alipokuta kuwa anaweza kuhukumu kitu kichungu kuwa ni kibaya na kitu kitamu ni kizuri na chenye muundo wa kutisha kuwa ni kibaya na chenye muundo mzuri kuwa ni kizuri, ameona kuwa anaweza kuhukumu juu ya ukweli kuwa ni uzuri na urongo kuwa ni ubaya na kutekeleza ahadi kuwa ni uzuri na khiyana kuwa ni ubaya. Akajipa nafsi yake jukumu la kuhukumu vitendo kuwa ni vizuri au vibaya bila kuangalia maudhui ya kheri na shari hilo halipatikani kwao katika hali hii na kujengea juu ya hukumu yake. Akaweka adhabu juu ya vitendo vibaya na akaweka tuzo kwa kitendo kizuri. Likaja sahihisho kwa hukumu hii kuwa kitendo hakipimwi juu ya kitu kwa sababu kitu kinachodirikiwa na hisia kwao ni chungu na tamu, cha kutisha au sura nzuri inayo mwezesha kuhukumu, kinyume na kitendo kisichopatikana kitu ndani yake anachokihisi mwanadamu hata aweze kuhukumu kuwa ni kibaya au kizuri. Haimkiniki kata kata kuvihukumu (vitendo) kuwa ni vizuri au vibaya kwa dhati yake. Basi

hapana budi kuchukuwa hukumu hii kwa mwengine naye ni Mwenyezi Mungu (swt). Uchunguzi huu ni juu ya hukumu juu ya kitendo sio katika upande wa vipimo; na uchunguzi hapa ni kwa upande wa adhabu juu ya vitendo na thawabu zake sio kwa upande wa kukitekeleza (kitendo) au kukipa nyongo (kukiwacha). Kwa hivyo kuna tofauti baina ya kheri (*khayr*) na shari (*sharr*) na baina ya zuri (*hasan*) na baya (*qabeeh*), na umekuwa ni maudhui mbili tofauti kabisa.

Huu ni kwa upande wa kusifu vitendo. Amma katika upande wa lengo la kitendo hapana budi kwa kila mwenye kutenda kitendo kuwa na kusudio (lengo) ambayo hutenda kwa ajili yake. Makusudio (malengo) hayo ndiyo thamani ya kitendo. Kwa hivyo ni lazima kwa kila kitendo kuwa na thamani ailengayo mwanadamu kuipata pindi anapotenda kitendo, na ikiwa hakuna (thamani inayolengwa) basi huwa ni mujarad wa kiholela. Haistahiki kwa mwanadamu kutenda vitendo vyake kiholela bila makusudio (lengo), bali hapana budi ila kuchunga kuhakikisha kupata thamani ya vitendo anavyo kusudia kutenda kwa ajili yake.

Na thamani ya vitendo ni imma iwe thamani ya ***kimada*** kama vitendo vya kibiashara, ukulima, usanii na mithali yake. Hakika linalo kusudiwa katika vitendo hivi ni kupatikana manufaa ya kimada kutokamano nazo nayo ni faida ambao ni thamani iliyo na uzito wake maishani. Na imma iwe thamani ya kitendo ni ***utu*** kama kuokoa waliozama na kuwasaidi wahitaji. Hakika linalokusudia katika kumuoka mwanadamu bila kuangalia rangi yake, jinsiya yake, dini yake au hisabu yeyote nyengine isiokuwa uwanadamu (utu). Na imma iwe thamani ya kitendo ni ya ***kiakhlaqi*** kama ukweli, uaminifu na huruma. Hakika linalolengwa kutokamana nayo ni upande wa *kiakhlaqi* bila kuangalia faida na bila kuangalia utu. Pia huenda ikawa akhlaqi pamoja na asiyekuwa mwanadamu kama upole kwa hayawani na ndege, na huenda ikapatikana hasara ya kimada kutokamana na kitendo cha akhlaqi lakini kukapatikana thamani yake ni wajibu nayo ni upande wa kiakhlaqi. Na imma iwe thamani ya kitendo ni ya ***kiroho*** kama ibadati. Sio linalokusudiwa kutokamana nalo faida ya kimada wala upande wa kiutu wala mas'ala ya kiakhlaqi bali linalokusudiwa kutokamana nalo ni mujarad wa ibadati kwa hivyo ni wajibu kuchunga kupatikana thamani yake ya kiroho tu bila kuangalia thamani nyenginezo.

Hizi ndizo thamani ya vitendo vyote, na ndizo mwanadamu hutenda vitendo ili kuzipata katika kila kitendo katika vitendo vyake.

Na vipimo vya mujtama za kibinadamu katika maisha yao ya duniani imma huwa kwa mujibu wa thamani hizi. Na vikapimwa (vitendo) kadri inapo patikana thamani hizi katika mujtamaa na inavyodhamini kupatikana kwao maisha mazuri na utulivu. Kwa hivyo ni juu ya Muislamu kutia juhudi zake ili

kuhakikisha thamani inayokusudiwa katika kila kitendo anachokitenda pindi anapokitenda kitendo hicho au kukiendea mbio mpaka achangie katika maisha mazuri ya mujtama na kuunyanyua, na kudhamini kwa wakati huo huo maisha mazuri kwake yeye na utulivu.

Na thamani hizi hazitenganiki wala hakuna usawa katika dhati zake kwa sababu hakupatikani baina yake sifa jumla yoyote ili ifanywe kuwa ni msingi wa kusawazisha kwa baadhi yake au kufadhilisha baadhi juu ya baadhi. Bali ni natija aliyokusudia mwanadamu pindi anapotenda kitendo. Kwa hivyo haimkiniki kuziweka katika mizani moja. Wala hazipimwi kwa kipimo kimoja kwa sababu hukhtalifiana ikiwa hazigongani. Isipokuwa mwanadamu ni katika hali yake kufadhilisha baina ya thamani ili achague iliyo bora, hata kama si bora au sawa, lakini mwanadamu haridhiki kwa hilo bali hufadhilisha na hufanya usawa baina yake. Na kufadhilisha huko na kufanya usawa haikujengwa juu ya nafsi ya thamani bali imejengwa juu ya yale yaliyomsibu kutokamana nayo. Na juu ya hayo mwanadamu kwa nafsi yake amejenga kufadhilisha na usawa baina ya thamani. Na kwa kinachopatikana kwake juu ya thamani hizi katika manufaa au madhara, kwa hivyo hufanya **nafsi** yake kuwa ni kipimo au kufanya athari ambayo husibu dhati yake katika thamani hizi kuwa ni kipimo. Na huwa kwa hakika ni kufadhilisha baina ya athari ya thamani kwa dhati yake kwa hivyo hukhtalifiana kufadhilisha kwao baina yake.

Watu ambao wameghilibiwa na hisia za kiroho na kumilikiwa na msukumo wake ni wenye kupuuza thamani ya kimada, wao hufadhilisha thamani ya kiroho juu ya thamani ya kimada na huelekea kwa ibadati na kuipa nyongo mada. Kwa hivyo hutweza maisha kwa sababu maisha ni mada na husababisha kuregea nyuma kwao kimada. Huporomoka kwa sababu yao mustawa (kiwango) cha mujtama wanaoishi ndani yake kwa kuenea ndani yake uvivu na ulegevu.

Na watu ambao wameghilibiwa na msukumo wa kimada na kumilikiwa na starehe na kupuuza thamani ya kiroho, wao hufadhilisha thamani ya kimada na huelekea kutaka kuipata. Kwa hivyo huzidi kwao muelekeo wa juu na mujtama wanaoishi ndani yake huchanganyikiwa kwa sababu yake, na huenea ndani yake shari na ufisadi.

Kwa haya imekuwa ni makosa kumwacha mwanadamu kupima thamani hizi bali ni wajibu kupimwa na Muumba wa mwanadamu naye ni Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo imekuwa hapana budi Shari'ah ndiyo impangie mwanadamu thamani hizi na kumpangia wakati wa kuzitenda, na kwa mujibu wake atazichukuwa mwanadamu.

Shari'ah imeshabainisha suluhisho la matatizo maishani kwa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo Yake, na akamlazimisha mwanadamu

kupeleka maisha haya kwa mujibu wa maamrisho na makatazo hayo. Pia amebainisha vitendo ambavyo huhakikisha thamani ya kiroho nazo ni ibadati ambazo alizoziwajibisha na za sunna. Pia amebainisha sifa ambazo hupatikana thamani ya ki-akhlaqi. Na akamwachia mwanadamu kuifikia thamani ya kimada ambayo humlazimu yeye ili akidhi dharura zake na mahitaji yake na yaliyo zaidi ya dharura katika mahitaji kwa mujibu ya nidhamu maalum aliyombainishia na kumwamrisha asiende kinyume nazo. Na hapana budi kwa Muislamu ila kutenda kwa ajili ya kufikia thamani hizi kwa mujibu ya maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo Yake na kupima (thamani hizo) kwa kipimo kilichokibainishwa *na Shari'ah*.

Kwa hivyo thamani hufikiwa katika mujtamaa kwa kiwango ambacho huitajia (thamani hiyo) kama mujtama maalumu. Na hupima mujtama huu kwa vipimo vyake na juu ya msingi huu ni wajibu kutenda vitendo kwa ajili ya kufikia/kupata thamani hizi ili ipatikane mujtama wa Kiislamu kwa mujibu wa mtazamo wa Kiislamu maishani.

Na kwa hayo huwa kitendo cha mwanadamu ni mada anachokitenda mwanadamu kimada. Isipokuwa yeye pindi anapokitenda kitendo hudiriki fungamano lake na Mwenyezi Mungu. Kwa hali ya kuwa kitendo ni halali au haramu, hukitenda au kujizuia kukitenda kwa msingi huu. Na huku kudiriki mwanadamu fungamano lake na Mwenyezi Mungu ndiyo roho, na ndiyo inayomlazimisha mwanadamu kujua Shari'ah ya Mwenyezi Mungu ili apimie vitendo vyake. Atafahamu kheri kutoka shari pindi anapojua yanayomridhisha Mwenyezi Mungu katika vitendo na yanayo mkasirisha Mwenyezi Mungu na atatofautisha baya (*qabeeh*) kutoka zuri (*hasan*) pindi Shari'ah inapomdokezea kitendo kizuri na kitendo kibaya. Na kwa haya humkinika kwake yeye pindi anapotenda kitendo na akadiriki fungamano lake kwa Mwenyezi Mungu asongea mbele kutenda kitendo au kuepukana nacho, kwa mujibu wa kudiriki huko kwa sababu yeye anajua aina ya kitendo na sifa yake na thamani yake. Na kufikia hapa imekuwa **falsafa ya Kiislamu ya kuunganisha mada na roho** yaani ni kufanya vitendo ni venye kupelekwa kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo Yake. Na imekuwa falsafa hii ni daima na lazima kwa kila kitendo jinsi kitakavyo kuwa kichache au kingi, kidogo au kikubwa. Na ikawa ndio mtazamo wa maisha. Inapokuwa aqeeda (itikadi) ya Kiislamu ndio msingi wa maisha, na ndio msingi wa falsafa na msingi wa nidhamu, hivyo basi huwa hadhara ya Kiislamu ni mkusanyiko wa fahamu juu ya maisha kwa mtazamo wa Kiislamu – iliojengwa (hiyo hadhara ya Kiislamu) juu ya msingi mmoja wa kiroho nayo ni *aqeeda (itikadi)*. Na ikawa mtazamo wake katika maisha ni kuunganisha mada na roho, na ikawa maana ya kupata mafanikio (*sa'ada*) katika mtazamo wake ni radhi za Mwenyezi Mungu.

Inapokuwa aqeeda (itikadi) ndio inayotatua tatizo kubwa nayo ndio msingi wa vitendo vya mwanadamu, na ndio inayosimama juu yake mtazamo wa kimaisha, na falsafa ambayo hudhibiti vitendo hivyo basi nidhamu ambazo zilizo tokamana na *aqeeda* ndio ambazo hutatua matatizo ya mwanadamu na kumpangia vitendo vyake kwa nidhamu kamili. Kwa hivyo imekuwa kutabikishwa kwake ni sehemu muhimu katika kupima hali ya serikali (*Dar*) kuwa serikali ya kikafiri au serikali ya Kiislamu.

Serikali ambayo hutabikishwa ndani yake nidhamu za Kiislamu na kuhukumiwa ndani yake kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, na kuwa amani/usalama wake ni kwa amani ya Kiislamu huwa ni serikali ya Kiislamu (*Dar ul-Islam*) hata kama wengi wa wakazi wake sio Waislamu. Na serikali isiyokusanya ndani yake mambo haya miwili huwa ni serikali ya kikafiri (*Dar ul-Kufr*) hata kama wengi wa wakaazi wake ni Waislamu.

Na kufikia hapa, la kutegemewa baada ya aqeeda kipao mbele ni juu ya nidhamu za Kiislamu na kwa kutabikishwa kwake katika kila nyanja ya maisha. Kwa sababu kutabikishwa kwa nidhamu hii pamoja na aqeeda hujenga katika Ummah akili ya Kiislamu (‘*aqqliyyah*) na hisia (*nafsiyyah*) za Kiislamu, ujengaji wa kimaumbile unaomfanya Muislamu kuwa na shaksiya ya hali ya juu ya kipekee.

Uislamu umekwisha mtazama mwanadamu kikamilifu bila kumgawanya vipande, na ukampangia vitendo vyake kwa hukumu za kiShari'ah mpango mmoja unaolingana, vyovyote yatakavyozidi na kutofautika vitendo hivi. Na hukumu hizi za kiShari'ah ndizo nidhamu za Kiislamu zinazo tatua matatizo ya mwanadamu. Isipokuwa pindi zinapo tatua matatizo yake huyatatua kwa hali ya kuwa kila tatizo lahitaji tatuo yaani kwa hali yake kama mas’ala yanayo hitajia hukumu ya kiShari'ah yaani hutatua matatizo yote kwa tatuo moja kwa sifa yake kama tatizo la kibinadamu sio kwa sifa yoyote nyengine. Nayo pindi inapotatua tatizo la kiuchumi mfano kama matumizi (*nafaqah*) au tatizo la utawala kama kumtawaza Khalifah au tatizo la kijamii kama ndoa, haizitatui kwa sifa yake kuwa ni tatizo la kiuchumi au kwa sifa yake kama tatizo la kiutawala au tatizo la kijamii bali huyatatua kwa sifa yake kama matatizo ya kibinadamu na hulivulia (*istinbat*) utatuzi yaani kwa hali yake kama mas’la yanayovuliwa kwake hukumu ya kiShari'ah. Uislamu una twarika (njia) moja ya kutatua matatizo ya mwanadamu nayo ni kufahamu tatizo linalo tokea na kuvua hukumu ya Mwenyezi Mungu juu yake kutokamana na dalili fafanuzi za kiShari'ah.

Na nidhamu za Kiislamu ni hukumu za kiShari'ah zinazo ambatana na ibadati, akhlaqi, vilaji, mavazi, maingiliano (*mu’malat*) na nidhamu za kuadhibu wahalifu.

Hukumu za kiShari'ah zinazo ambatana na ibadati, akhlaqi, vilaji na mavazi hazina *'illa* (sababu ya kiShari'ah ya kuteremshwa hukumu).

Mtume (saw) alisema:

**حرمت الخمر لعينها**

*"**Imeharamishwa tembo (khamr) kwa asili yake**."*

Amma hukumu za kiShari'ah zinazo ambatana na maingiliano na nidhamu za kuadhibu wahalifu, hizo zina *'illa* kwa sababu hukumu za kiSheri'ah juu yake zimejengwa juu ya *'illa* iliyo sababisha kuwekwa hukumu kwa ajili yake. Hakika wamezowea wengi kuweka *'illa* ya kimanufaa kwa ahkamu zote kwa kuathirika na fikra kiongozi ya kimagharibi na hadhara ya kimagharibi ambayo hufanya manufaa pekee kuwa ni kipimo/msingi cha vitendo vyote. Haya hugongana na fikra kiongozi ya Kiislamu inayofanya roho kuwa ndio kipimo/msingi wa vitendo vyote, na kuunganishwa kwake na mada ndio inayodhibiti vitendo. Na kwa haya hakika wa hukumu za kiShari'ah zinazo ambatana na ibadati, akhlaqi, vilaji na mavazi hazina sababu kata kata kwa sababu hukumu hizi hazina *'illa.* Bali huchukuliwa tu kama zilivyopokewa na dalili wala hazijengwi kata kata juu ya *'illa*. Swala, saumu, hijja, zakaa, jinsi ya kuswali na idadi ya rakaa zake, amali za hijja, nisabu ya zaka na mithali/mifano yake huchukuliwa vile vile kama zilivyokuja (*tawqeefiyyah*), na hupokelewa kwa kukubaliwa na kusalimu amri bila ya kuangalia *'illa* yake bali hata haitafutwi *'illa* yake. Hivyo hivyo kuharamishwa kwa mfu, nyama ya nguruwe na yasiyokuwa hayo milele haitafutwi *'illa* yake bali ni katika makosa na hatari kutafutwa *'illa* kwa sababu lau ingelitafutwa *'illa* za ahkamu za vitu hivi natija yake ni lau hino *'illa* itapotea basi hukumu itapotea kwa sababu *'illa* huzunguka na kile kinachofanyia kazi (*ma'lul*) kwa kuweko na kutokuweko. Kwa mfano Lau tutalazimisha kuwa *'illa* ya udhu ni usafi na *'illa* ya swala ni mazoezi na *'illa* ya saumu ni afya na mifano yake, natija yake itakuwa kwamba ikipotea *'illa* basi hukumu haitokuwepo ilhali mambo si hivyo. Kwa hivyo imekuwa ni hatari kwa hukumu kutafutiwa *'illa* ya kuitenda. Ni wajibu kuchukuliwa hukumu za ibadati kama zilivyo bila kuzitafutia *'illa*. Amma kuhusu *hekima* (iliyoko nyuma ya hukumu), ni Mwenyezi Mungu pekee ndiye anayeijua na akili zetu haziwezi kudiriki uhakika wa dhati ya Mwenyezi Mungu basi hatuwezi kudiriki *hekima* yake. Amma *hekima* zilizopokewa kutokamana na dalili kama msemo Wake (swt):

**{ إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَى عَنْ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ }**

**"*Hakika Swala inazuilia mambo machafu na maovu*"** [Al-'Ankabut 29: 45]

Na msemo Wake (swt):

**{ لِيَشْهَدُوا مَنَافِعَ لَهُمْ }**

**"*Ili washuhudie manufaa yao*"** [Al-Hajj 22: 28]

Na msemo Wake (swt):

**{ وَمَا آتَيْتُمْ مِنْ زَكَاةٍ تُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُضْعِفُونَ }**

**"*Na mnachokitoa kwa Zaka kwa kutaka radhi ya* Mwenyezi Mungu*, basi hao ndio watakao zidishiwa*"** [Ar-Rum 30: 39]

Na hekima nyenginezo zilizotajwa wazi na dalili, hizi zakoma juu ya dalili na huchukuliwa jinsi zilivyo wala haizidishiwi juu yake. Na isiyothubutu kwa dalili basi haitafutiwi hekima kama isivyotafutiwa *'illa*.

Hii ni katika upande wa ibadati. Amma akhlaqi, hizo ni thamani zilizojaaliwa ahkamu zilizo bainisha fadhila na akhlaqi njema na zilizo kinyume nazo. Kama zilivyo jaaliwa kuwa ni natija ya ibadati na yanayo lazimika kuzingatiwa katika maingiliano. Hii ni kwa sababu Uislamu umelenga katika Shari'ah zake kumpeleka mwanadamu katika njia ya ukamilifu mpaka afikie katika daraja ya juu kabisa anayoweza, na ina pupa asifike na sifa ya juu na abakie akisifika nazo. Akhlaqi njema ni thamani zinazo chungwa kutekelezwa pindi anaposifika nazo nayo huhusika na zile fadhila zilizotajwa wazi na Shari'ah, na huchungwa thamani yake pindi anapotenda fadhila hiyo na anaposifika nayo. Akhlaqi ni sehemu ya Shari'ah ya Kiislamu na ni sehemu ya maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo Yake ambayo hapana budi zifikiwe katika nafsi ya kila Muislamu ili atimize amali zake na akamilishe Uislamu wake na kutenda kwake kwa mujibu ya maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo Yake.

Mwislamu hasifiki na sifa za kiakhlaqi kwa dhati zake wala si kwa sababu ya manufaa yaliyomo ndani yake, bali husifika nazo tu kwa sababu Mwenyezi Mungu ameziamrisha si kwa sababu ya kitu chengine chochote. Hasifiki Muislamu kwa ukweli kwa sababu ya dhati ya ukweli wala si kwa sababu ya manufaa yaliyomo ndani yake bali ni kwa sababu Shari'ah imemuamrisha nao.

Amma kutosifika Muislamu na akhlaqi kwa sababu ya dhati ya akhlaqi, hilo huregelea sifa ya vitendo. Huenda ikawa kitendo ambacho amekitenda mwanadamu kwa dhati yake ni kiovu na yeye akidhania ni chema na akitende. Na huenda kuwa sifa ambazo wanasifika nazo wanadamu kwa dhati yake ni sifa za uovu lakini wakadhania ni sifa njema na kuzibeba na hivyo makosa huchipuza kutokana na mwanadamu kutenda kwa dhati ya akhlaqi.

Na kisichodokezwa na Uislamu kuwa ni sifa njema na sifa mbaya na akazitenda mwanadamu kwa msingi wa ufafanuzi huu, haimkiniki kuwa kusifika kwake na sifa hizi imelingana na hukumu za kiShari'ah. Kwa hivyo haijuzu kwa Muislamu kusifika na ukweli kwa dhati ya ukweli wala haurumii wanyonge kwa dhati ya huruma, wala hasifiki na akhlaqi kwa dhati ya akhlaqi

bali husifika nazo kwa sababu Mwenyezi Mungu amemuamrisha nazo. Kwa sababu hakika za akhlqai hizi hutegemea juu ya *aqeeda* (itikadi) ya Kiislamu, na hichi ndicho kitu cha undani wake. Na hii ndiyo hutosheleza kumakinisha akhlaqi katika nafsi na kubakia kwake kuzisafisha kutoka kila uchafu, na kuiweka mbali na kila sababu za kuzifisidi. Kwa hivyo imekuwa kinga ya akhlaqi kwa nafsi ni kujifunga na yaliyokuja ya dalili, na kufungika katika msingi wa kiroho na kujengwa juu ya aqeeda ya Kiislamu.

Amma kutosifika mwanadamu na akhlaqi kwa sababu ya yaliyomo ya manufaa ndani yake hilo huregelea kuwa manufaa sio linalokusudiwa katika akhlaqi wala haijuzu kuwa ndiyo iliyokusudiwa ili isifisidike (akhlaqi) na ili isizunguke nayo popote inapozunguka manufaa. Akhlaqi ni sifa ambazo hapana budi kwa mwanadamu kusifika nazo kwa utiifu na khiyari kwa msukumo wa uchajimungu. Na Mwislamu hatendi vitendo vya kiakhlaqi kwa sababu hunufaisha au hudhuru maishani bali huvitenda kwa kuitikia maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu. Hili ndilo linalofanya kusifika kwa akhlaqi njema ni yenye kudumu na thabiti isizunguke panapo zunguka manufaa.

Akhlaqi hizi zinazosimama juu ya kubadilishana manufaa humfanye mwenye kuzitenda kuwa ni mnafiki. Huwa ndani yake sio dhahiri yake kwa sababu akhlaqi kwake imejengwa juu ya manufaa na huzunguka katika nafsi yake pale panapo zunguka manufaa kwa sababu mwanadamu huzungusha hukumu zenya *'illa* juu ya *'illa* zake wala haitakidi kuwepo kwake wala uwajibu wake pindi anapoona kuwa sababu yake imeondoka.

Kwa hivyo zimekuwa akhlaqi hazina *'illa* wala haijuzu kuwekewa *'illa* bali huchukuliwa kama Shari'ah ilivyokuja nazo bila kuangalia *'illa* yoyote miongoni mwa *'illa*. Ni katika makosa na hatari akhlaqi kuwekewa *'illa* ili isibatilike kusifika nazo kwa kupotea *'illa* yake.

Kufikia hapa hubainika kuwa makusudio ya ibadati ni thamani ya kiroho pekee na makusudio ya akhlaqi ni thamani ya kiakhlaqi pekee, na ni wajibu kubakia kwa thamani hizo zilizokusudiwa sio nyengine. Haijuzu kubainisha yaliyomo katika ibadati na akhlaqi miongoni mwa faida na manufaa kwa sababu kubainisha hivi ni hatari kwake kwa kusababisha unafiki katika wenye kuabudu na walio na akhlaqi, na hupeleka kuwachwa kwa ibadati na akhlaqi pindi isipo dhihiri faida yake wala kuonyesha wazi manufaa yake.

Amma hukumu za kiShari'ah zinazoambatana na vitendo vya mwanadamu katika mafungamano yake pamoja na mwanadamu mwengine, miongoni mwa dalili zilizokuja nazo hukusanya *'illa* kama msemo Wake (swt) katika kuwapa ngawira (*fai*) ya Banu Nadhir kwa muhajirina bila maansari:

كَيْ لاَ يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ

**"*ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri miongoni mwenu*"**

[Al-H'ashri 59: 7]

Na nyengine zisizokusanya *'illa* ni kama msemo Wake (swt):

وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا

**"Mwenyezi Mungu *ameihalalisha biashara na ameiharamisha riba*"**

[Al-Baqarah 2: 275]

Hivyo basi hukumu yoyote ambayo dalili yake imejumuisha *'illa* hufanyiwa kipimo (*qiyas) juu yake*. Yaliyokuja kutoka dalili zisizokuwa na *'illa* basi haziwekewi *'illa* kata kata na hazifanyiwi *qiyas*. Na *'illa* inayo tambuliwa ni *'illa* iliyowekwa na Shari'ah yaani iliyodokezwa na dalili ya kiShari'ah kutokamana na *Kitabu* na *Sunna* kwa sababu hizi mbili ndizo dalili za kiShari'ah pekee. Kwa hivyo *'illa* inayojengwa juu yake hukumu ya kiShari'ah iliyo na *'illa* ni *'illa* ya kiShari'ah wala sio *'illa* ya kiakili yaani ni wajibu iwe imekuja kwa dalili iliyo wazi (*sareeh*) au kwa kudokezwa (*dalalah*) au kwa kuvuliwa (*istinbat*) au kwa kupimwa (*qiyas*). *'Illa* hino huzunguka pale inapozunguka kilichowekewa *'illa* kwa kuwepo na kutokwepo basi hukumu huzunguka na *'illa* yake pindi inapozunguka. Utaona kitu kimoja kinakatazwa katika hali (fulani) kwa sababu ya *'illa* ya kiShari'ah, na pindi inapoondoka *'illa* hiyo haijuzu kitu hicho basi hukumu ya kiShari'ah huzunguka pamoja na *'illa* inapokuwepo na kutokuwepo. Inapopatikana *'illa* hupatikana hukumu na inapokosekana *'illa* hukosekana hukumu.

Isipokuwa kuondoka hukumu kwa sababu ya kuondoka *'illa* yake haimanishi kata kata kuwa hukumu imebadilika bali hukumu ya kiShari'ah juu ya mas'ala ni hiyo hiyo haibadiliki. Bali hukumu haitekelezwi tu pindi inapoondoka *'illa* yake na hutekelezwa hukumu kwa kurudi *'illa* yake.

Mahusiano ya hukmu na *'illa* katika kuwepo kwake na kutokwepo kwake haimaanishi kuwa hukmu hiyo imebadilika kwa kubadilika zama na mahali kwa mwito wa kuwa kupata maslahi na kuepusha ufisadi (*jalab al-masalih wa dar'u al-mafasid*) kuwa ndio *'illa* ya hukmu za kiShari'ah, inayobadilika kwa kubadilika zama na mahali basi hubadilika hukmu kwa kubadilika kwake. Hilo ni kwa sababu kupata maslahi na kuepusha ufisadi sio *'illa* kata kata ya hukmu za ki-Sheria kwa sababu haijakuja dalili kudokeza kuwa kupata maslahi na kuepusha ufisadi ndio *'illa* ya humu za kiShari'ah. Wala haijakuja dalili yoyote inayoidokeza kuwa ni *'illa* ya hukmu maalumu basi haiwi ni *'illa* ya kiShari'ah.

*'Illa* ya kiShari'ah ni ile tu iliyodokezwa na dalili ya kiShari'ah basi hapana budi kujifunga nayo na kusimama (kukoma) kwa maana yake, nayo haidokezi

kuwa kupata maslahi na kuepusha ufisadi. Basi huwa *'illa* ya kiShari'ah ni ile iliyokuja nayo dalili ya kiShari'ah wala sio kupata maslahi na kuepusha ufisadi. Na iliyokuja nayo dalili haikudokeza juu ya zama na mahali, wala haidokezwi na dhati ya kitendo, bali imedokezwa na dalili ya kiShari'ah katika kubainisha *'illa* ya hukmu, na dalili hiyo kata kata haibadilishwi basi haizingatiwi kubadilika kwa zama na mahali katika maudhui haya wala hakuna thamani ya kupata maslahi na kuepusha ufisadi.

Kwa hivyo, hukmu za kiShari'ah hazibadiliki kwa kubadilika zama na mahali bali hukmu ya kiShari'ah ni ile ile haibadiliki vyovyote itakavyo badilika zama na mahali.

Amma kubadilika desturi na ada za watu, hilo haliathiri katika kubadilisha hukmu kwa sababu desturi sio *'illa* ya hukmu wala si msingi wake. Desturi imma imekhalifu Shari'ah au haikuikhalifu. Ikiwa zimekhalifu Shari'ah basi Shari'ha imekuja kuzifuta na kuzibadilisha kwa sababu miongoni mwa kazi za Shari'ah ni kubadilisha desturi na ada mbovu kwa sababu ndio zinazo sababisha kuharibika kwa mujtama. Kwa hivyo haichukuliwi kuwa ni msingi wa hukmu ya kiShari'ah wala sio *'illa* yake, na haibadiliki hukmu kwa ajili yake. Na ikiwa haikhalifu Shari'ah, hukmu huthibitika kwa dalili yake na *'illa* yake ya kiShari'ah sio kwa desturi hizo hata kama hazikhalifu Shari'ah. Kwa hayo ada haihukumu juu ya Shari'ah bali Shari'ah huhukumu juu ya ada na desturi. Basi hukmu za kiShari'ah dalili yake ni *nass* na zina *'illa* ya kiShari'ah, na desturi na ada sio katika hizo kata kata.

Amma kuhusu kufaa kwa Shari'ah ya Kiislamu kwa kila zama na mahali, hilo hutokamana na upande wa kuwa Shari'ah ya Kiislamu hutatua matatizo ya mwanadamu katika kila zama na mahali kwa hukmu zake, na ni pana kwa kutatua matatizo yote ya mwanadamu jinsi yatakavyo kuwa mapya na kutofautika kwa sababu Shari'ah pindi inapotatua matatizo ya mwanadamu hutatua kwa sifa yake kama mwanadamu wala si kwa sifa nyengine.

Na mwanadamu hubakia kuwa mwanadamu katika kila zama na mahali katika upande wa ghariza zake na mahitaji yake ya kiviungo wala habadiliki milele. Hivyo hivyo hukmu za kuzitatua hazibadiliki; kinachobadilika ni muundo wa maisha ya mwanadamu na hili haliathiri katika mtazamo wake maishani. Amma yanayokuwa mapya katika matakwa tofauti tofauti ya mwanadamu, hilo hutokamana na ghariza hizo na mahitaji ya kiviungo, na imekuja Shari'ah iliyo pana kutatua matakwa hayo yaliyo mapya na yanayo tofautika jinsi yatakavyo badilika na jinsi yatakavyo badilika muundo wake. Na hilo limekuwa sababu miongoni mwa sababu zilizoikuza fiqhi. Isipokuwa upana huo katika Shari'ah haimaanishi kuwa ni 'kupanuliwa (Shari'ah)' kwa hali yakuwa inatabikishwa juu ya kila kitu hata kama inagongana nayo. Wala haimaanishi kuwa ni yenye kubadilika kwa hali ambayo hubadilika pamoja na

zama bali humaanisha upana wa dalili ili kuvua (*istinbat*) hukmu tofauti tofauti na pia humaanisha upana wa hukmu ili kutabikishwa juu ya mas'ala mengi.
Mfano husema Allah (swt):

فَإِنْ أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ

**"*Na wakikunyonyesheeni basi wapeni ujira wao*"** [At-Talaq 65: 6]

Hakika aya hii huvuliwa kutokamana nayo hukmu ya kiShari'ah nayo ni mwanamke aliyepewa talaka yuwastahiki ujira wa kunyonyesha na huvuliwa kutokamana nayo pia hukmu ya kiShari'ah kuwa yeyote aliyeajiriwa anastahiki ujira anapofanya kazi yake sawa sawa awe ameajiriwa na mtu binafsi au ameajiriwa na watu jumla (*ajeer 'amm*). Hukmu hii hutabikishwa juu ya mas'ala mengi miongoni mwake mfanyikazi wa serikali, mfanyikazi katika kiwanda, mkulima katika shamba na wanaofanana nao hustahiki kila mmoja wao ujira wake anapo maliza kazi yake kwa sababu yeye ni muajiriwa binafsi (*ajeer khas*s). Na seremala ambaye hutengeneza kabati, mshonaji ambaye hushona nguo na mtengeneza viatu anaye tengeneza viatu na mifano yao hustahiki kila mmoja wao ujira wake anapo tenda kazi yake kwa sababu yeye ni muajiri jumla (*ajeer 'amm*). Na kwa kuwa kuajiriwa ni mkataba baina ya mwenye kuajiri na aliyeajiriwa, haingii ndani yake mtawala (*haakim*) kwa sababu yeye hakuajiriwa na Ummah bali yeye ni mwenye kutekeleza hukmu za kiShari'ah yaani mwenye kutabiksha Uislamu. Kwa hivyo hastahiki Khalifah ujira kwa kutenda kazi yake kwa sababu yeye amepewa bay'ah (ahadi ya utiifu) ili azitekeleze Shari'ah na kubeba ulinganizi wa Kiislamu naye hakuajiriwa na Ummah. Hivyo hivyo wasaidizi wake ambao ni viungo katika idara ya utendaji na mawali hawastahiki ujira kwa kutenda kazi zao kwa sababu kazi zao ni utawala (hukmu) na wao sio waajiriwa. Kwa hivyo hawachukuwi ujira bali hukadiriwa makadirio yatakayo tosheleza mahitaji yao kwa sababu ya kushughulishwa kutotekeleza mambo yao ya kibinafsi na ajira.

Upana huu wa dalili wa kuvua hukmu nyingi na upana wa hukmu unaotabikishwa juu ya mas'ala mengi ndio ambao unaofanya Shari'ah ya Kiislamu kutosheleza katika kutatua matatizo yote ya maisha katika zama zote na mahala na kila Ummah na karne, wala huku sio kupanuliwa wala kubadilika (kwa Shari'ah).

Na dalili ya hukmu za ki-Sheria zilichochukuliwa kutoka *nass* ya Kitabu na Sunna hutatua matatizo yaliyotokea kwa sababu Mteremshaji Shari'ah (*Ash-Shari'*) amekusudia kufuatwa maana ya *nass* wala sio kusimama juu ya maana ya kilugha ya *nass.* Hivyo basi, wakati wa kuvua hukmu ya kiShari'ah umuhumi huelekezwa kwa maana ya '*illa (dalili ya kiShari'ah).*

Na dalili yaweza kujumuisha *'illa* ya hukmu au *'illa* yaweza kuchukuliwa kutoka kwa dali moja au zaidi. Na hata kama imevuliwa kutokamana na dalili yake lakini huchungwa ndani yake upande wa *'illa* pasina na kuzingatia mtazamo

uliotajwa katika dalili iliyokuja kutatua tatizo wakati ule. Mfano ni msemo wa Mwenyezi Mungu (swt0

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهِبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ

***"Waandalie (jeshi) lenye nguvu muwezavyo na farasi walio fungwa tayari-tayari, ili kuwatishia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu"***

[Al-Anfal 8: 60]

**Hukmu** ni kuandaa nguvu na miongoni mwake ni vipando vya farasi. **Na upande wa *'illa*** katika hukmu ni kutishia adui. Pindi inapovuliwa leo kutoka dalili hukmu ya maandalizi ya nguvu, tutachunga upande wa *'illa* katika hukmu na tutaandaa yale yatakayo hakikisha utisho kwa adui. Wala hatufungwi na yaliyotajwa na dalili (ambayo ni kuandaa vipando vya farasi) katika kutatua tatizo lililokuwa wakati ule.

Huu ndio mtazamo unaofuatwa katika kila dalili inayovuliwa kutokamana nayo hukmu kwa sababu muradi wake ni kuhakikishwa upande wa *'illa* katika hukmu. Kwa hivyo Shari'ah ya Kiislamu imeweka katika hukmu zinazo ambatana baina ya watu katika maingiliano (*muamalat*) kwamba zijengwe juu ya *'illa*, na kuchungwa katika dalili wakati wa kuvua hukmu kutokamana nayo upande wa uteremshaji Shari'ah (*tashri'*) na wala sio sura iliyopokewa katika dalili.

Kama inavyokuwa dalili ya Kitabu na Sunna ni dalili ya kiSharia juu ya hukmu, hivyo hivyo Ijma'a (waliyokukubaliana/waliyoafikiana) ya Maswahaba na *qiyas* huhisabiwa miongoni mwa dalili za kiShari'ah. Kwa hivyo dalili za kiShari'ah za kijumla kwa hukmu za kiShari'ah ni *Kitabu*, *Sunna*, *Ijma'a as-Sahabah* na *qiyas*. Amma *madhab* ya sahaba *(rai ya swahaba*) mmoja katika mas'ala ya kiijtihadi, haiwi ni dalili ya kiShari'ah kawa sababu sahaba ni mujtahid mwengine na ana uwezekano wa kukosa. Na kwa kuwa masahaba wamekhtalifiana katika masa'la na akaenda kila mmoja wao kinyume na *rai* ya mwengine, na lau ingefanywa *rai* ya sahaba mmoja kuwa ni hoja zingekuwa hoja za Mwenyezi Mungu ni zenye kukhtalifiana na kugongana. Kwa hivyo haihisabiwi *rai* ya sahaba kuwa ni dalili ya kiShari'ah bali yajuzu kuchukua kutoka kwake kama rai nyinginezo za *madhab* zinazo tambuliwa. Amma waliyoafikiana juu yake Maswahaba katika hukmu, hiyo si *madhab* kwao wao bali huwa ni *Ijma'a*.

Amma Sheria ya watu kabla yetu, haihisabiwi kuwa ni Sheria kwetu sisi wala haihisabiwi miongoni mwa dalili (chimbuko) za kiShari'ah. Hata kama aqeeda ya Kiislamu yawajibisha imani kwa Mitume (*anbiyaa*) na Wajumbe (*rusul*) wote na kwa vitabu ambavyo vimewashukia. Lakini maana ya imani kwao wao ni kusadikisha kwa utume wao na ujumbe wao na kwa yaliyo washukia katika vitabu, wala sio maana ya imani kwao wao ni kuwafuata, kwa sababu

baada ya kutumilizwa Muhammad (saw) wamekuwa watu wote ni wenye kuamrishwa kuwacha dini zao na kufuata Uislamu kwa sababu haihisabiwi dini yoyote isiyokuwa dini ya Uislamu. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الإِسْلاَمُ

***"Hakika dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu."*** [Aal-e-Imran 3: 19]

Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الإِسْلاَمِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الآخِرَةِ مِنْ الْخَاسِرِينَ

**"*Anayetafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara*"** [Aal-e-Imran 3: 85]

Ayah hii iko wazi (sareeh) katika maana. Kutokana na Ayah hii kukapatika qaida (msingi) hii:

شرع من قبلن ليس شرعا لنا

***'Sheria ya watu kabla yetu sio Sheria kwetu.'***

Na dalili nyengine juu ya *qaida* hii ni kuwa Masahaba wameafikiana (*ijma'a*) kuwa Shari'ah iliyomshukia Muhammad (saw) imezifuta Sheria zote zilizotangulia kwa sababu Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنْ الْكِتَابِ وَمُهَيْمِنًا عَلَيْهِ

**"*Na tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Vitabu na kuyalinda.*"** [Al-Ma'idah 5: 48]

Yaani (Qur'an) yenye kutawala na iliyo juu. Na hukmu ya Qur'ani kuwa juu ya vitabu vilivyo tangulia ni kuzifuta Sheria zilizotangulia yaani imekuja kusadikisha na kuzifuta. Na imepokewa kutoka kwa Mtume (saw) kuwa alimuona Umar bin Al-Khattab akiwa na kipande cha Taurati akiitizama basi akakasirika na akasema:

ألم آت بها بيضء تقية ولو أدر كني أخي موسى لما وسعه إلا إتباعي

*"**Je, sikuja na yaliyo meupe na safi? Na lau angelikutana na mimi ndugu yangu Musa asingekuwa na khiyari ila kunifuata mimi**."*

Pamoja na kuwa amali za Hajj kama *Tawaf* pambizoni mwa *Ka'abah*, kugusa jiwe jeusi na kubusu na kufanya *say* baina *Safa* na *Marwa* zilikuweko katika zama za *ujahiliyya*, pindi sisi tunapozitenda na kuabudu nazo hatuzitenda kama amali ya Sheria zilizotangulia bali twazitenda tukizihisabu kuwa ni Shari'ah ya Kiislamu kwa sababu Uislamu imekuja nazo kama hukmu za kiShari'ah mpya wala sio kukiri Sheria zilizotangulia. Hivyo hivyo yote yaliyokuja kutoka dini zote zilizo tangulia, hatuzitekelezi kattu; bali twatekeleza iliyokuja nayo Shari'ah ya Kiislamu tu. Kwa hivyo huwa mnasara

na mayahudi ni wenye kukhutubiwa na Shari'ah ya Kiislamu na ni wenye kuamrishwa kuwacha Sheria zao kwa sababu Uislamu umezifuta Sheria zao. Na ikiwa hilo ni wajibu kwa wafuasi wa Sheria ya kiyahudi nao ni mayahudi na manasara, basi vipi Muislamu huombwa (*huamrishwa*) kuchukuwa Sheria ya walio kabla yake kuwa ni Sheria yake?

Mwenyezi Mungu (swt) asema:

إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ

"***Tumekuletea wahyi wewe kama tulivyo wapelekea wahyi Nuhu***"

[An-Nisa' 4: 163]

Muradi wake ni kuwa ameteremshiwa (Muhammad) wahyi kwake kama walivyo teremshiwa wahyi kwa wengineo miongoni mwa Mitume. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

شَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ نُوحًا

"***Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu***"

[Ash-Shura 42: 13]

Maana yake ni kwamba kupewa (Muhammad) Shari'ah ya asili ya tawhid nayo ndiyo aliousiwa nayo Nuhu. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَنِ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا

"***Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim***"

[An-Nahl 16: 123]

Maana yake ni kufuata asili ya tawhid kwa sababu '*mila*' maana yake ni asili ya tawhid. Na muradi wa aya hizi zote na zilizo fanana nazo ni bayana kuwa yeye (saw) sio mzushi katika utume bali ametumwa kama walivyotumwa wengineo, na kuwa asili ya *tawhid* ndiyo dini na ndiyo walioshirikiana nayo Mitume na Wajumbe wote. Amma yasiyokuwa hilo kila Mjumbe ametumwa na dini khaswa. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

لِكُلٍّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَاجًا

"***Kila mmoja katika nyinyi tumemwekea Shari'ah yake na njia yake***"

[Al-Ma'idah 5: 48].

Kwa hilo, hakika Sheria za wale waliotangulia kabla yetu sio Sheria kwetu wala haihisabiwi miongoni mwa dalili (chimbuko) za kiShari'ah ambazo huvuliwa kutokamana nazo hukmu.

Asili katika kuvua hukmu ni kwa *mujtahidina* kwa sababu ujuzi wa hukmu ya Mwenyezi Mungu katika mas'ala haiwi ila kwa *ijtihadi*; kwa hivyo hapana budi ila kuwepo kwa *ijtihadi*. Na wamesema wanavyuoni wa misingi (*usul*) kuwa ijtihadi ni faradhi ya kutosheleza (*fard kifaya*) juu ya Waislamu na haijuzu kwa

zama miongoni mwa zama kukosekana *mujtahid*. Na ikiwa (Waislamu) wote wameafikiana kuiwacha *ijtihadi* ni dhambi, na hilo ni kwa sababu njia ya kujua hukmu za kiShari'ah ni kupitia *ijtihadi*. Na lau ingekosekana zama kuwepo mujtahid mwenye kutegemewa katika kuvua hukmu, hii hupelekea kuwachwa kwa hukmu za kiShari'ah na hilo halijuzu. Isipokuwa *ijtihadi* ina shuruti zake zilizo fafanuliwa na maulama wa *usul.* Yahitaji (*ijtihadi*) mtazamo mpana, ufahamu wa sahihi kwa dalili (*nusus*) na ujuzi kamili wa lugha ya kiarabu. Na huhitajia kuifahamu fiqhi (mas'ala ya kiShari'ah) na kusimama juu ya dalili zake.

Kwa hivyo kuvua hukmu bila mazingatio wala mtazamo mzuri hauitwi kuvua (*istinbat*), kama vile ambavyo hauitwi mujarad ya kudhihiri *maslahi* katika hukmu kisha kufanya ujanja juu ya dalili na kuzibebesha yasiyo kusudiwa nayo ili kustanbiti (kuvua) hukmu hiyo kuwa ni *ijtihadi*. Bali hilo ni kuitukana (kuikosea) dini ya Mwenyezi Mungu inayostahiki aliyeitenda adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Ni kweli kuwa mlango wa ijtihadi uko wazi lakini uko wazi kwa maulama sio kwa wajinga. *Mujtahidina* ni aina tatu: Mujtahid *mutlaq*, mujtahid *madhab* na aina hizi mbili zina shuruti maalumu. Amma watatu, huyu ni mujtahid wa suala moja (*mujtahid mas'alah)*, naye ni mwenye uweza wa kufahamu dalili na kulifuata suala moja na dalili zake na dalili za *mujtahidina* wengine juu yake. Nayo (aina hii ya ijtihad) ni lazima kwa kila Muislamu anayetaka kujua hukmu ya Mwenyezi Mungu. Hakika Shari'ah imefanya asili ya kila Muislamu achukuwe hukmu kwa nafsi yake kutokamana na dalili yaani awe *mujtahid* katika dini katika mas'ala ambayo yanamlazimu.

Lakini baada ya kurekodiwa *madhab* ya mujtahidina na kumakinishwa nguzo (*qawa'id*) za hukmu, fikra ya ijtihadi ilidhoofika katika nyoyo na *mujtahidina* wakawa wachache. Ikazidi kwa Waislamu wengi *taqleed* na ikawa ni nadra ijtihadi kwa Waislamu, mpaka ikavuka mipaka fikra ya *taqleed* mpaka wakatokea wenye kusema kufungwe mlango wa ijtihadi na kuzungumzia uwajibu wa *taqleed*. Kwa ajili ya hayo watu wengi miongoni mwa Waislamu kama si wote wakawa *muqallideen* (wafuasi wa mujtahidinna)

Na *muqallid* ni vigawanyo viwili: *muttabi'a* na *'aammi*. Tofauti baina ya *mutabi'a* na *'aammi* ni kuwa ***muttabi'a*** huchukuwa hukmu ambayo imevuliwa na mujtahid mmoja baada ya kukinaika kwake kwa dalili ambazo amezitegemea (*mujtahid*) wala hamfuata bila kuijua dalili zake. Na *'**aammi*** ni mwenye kumfuata mujtahid katika hukmu za kiShari'ah bila ya kuchunguza dalili. Na *muttabi'a* ni hali bora kuliko *'aammi*, na walikuwa wengi katika waliotangulia katika *muttabi'a* kwa kujali kwao kuzisoma dalili. Ilipokuja zama za mporomoko na ikawa ngumu kwa watu kufuata (*itiba'a*), wakawa wakifanya *taqlid* kwa maimamu na *mujtahidina* kwa hukmu bila ya

kuchunguza dalili. Kilicho washajiisha wao kwa hilo ni kunyamaza kwa *maulam*a na kuridhia kwao watu kuwa *‘aammi* hata kama ni katika wenye kusoma. Na sababu ya kunyamaza *maulamaa* juu ya hilo ni kuwa *taqleed* kwa asili yake yajuzu sawa sawa akiwa *muqallid* ni *muttabi'a* au *‘aammi*. Isipokuwa asili kwa Muislamu ni kuchukua hukmu kutokamana na dalili yake lakini yajuzu kwake yeye kuwa *muqallid* na yajuzu kwake yeye kuwa *muttabi'a* yaani kujua hukmu na kujua dalili zake na kukinaika nayo. Na hino ndio inayomfanya Muislamu awe mtu wa *ijtihad* hata kama kwa suala moja, na hili latulazimu sisi katika zama zetu hizi. Na *fatwa* sio katika mlango wa *ijtihadi* kwa sababu haiingii katika *ijtihadi* bali ni aina duni zaidi ya utungaji katika *fiqhi*. Hilo ni kuwa limetokea baada ya zama za *mujtahidina* na zama za wanafunzi wao na wanafunzi wa wanafunzi wao. Hawa wakaelekea katika kusherehesha rai za *madhab* na kubainisha msingi wake na kuzimakinisha rai zake, na huhisabiwa zama hizo kuwa ni zama za waridi (iliyo nawiri) kwa fiqhi. Zilitungwa katika zama hizo vitabu mama vya fiqhi katika *madhab* tofauti na ndizo zinazo hisabiwa kuwa ni maregeo kwa mas’ala ya kifiqhi. Hayo yakaendelea mpaka karne ya saba hijri, kisha ikaja baada yake zama za mporomoko wa *kifiqhi* nayo ni zama za kusherehesha na ufafanuzi. Na nyingi wa zama hizi zilikuwa tupu kwa uvumbuzi, *istinbati* na ijtihadi hata katika suala moja. Kisha ikaja baada yake zama za mporomoko zaidi, wakaja katika zama hizo *maulama* walioingilia katika njia ya kutaja mas’ala na hukmu bila kulenga sura zake na vitagaa vyake, na zikaitwa mas’ala hayo kuwa ni *fatwa*. Kwa hivyo hazisihi kuchukuliwa kuwa ni maregeo kwa hukmu, kama haisihi kuchukuliwa fatwa hizi kuwa maregeo ya hukmu za kiShari'ah kwa kuwepo kwao mbali na njia ya ijtihadi katika kuvua (*istinbat)* hukmu.

Hivyo hivyo haijuzu kuchukuliwa kama maregeo ya hukmu za kiShari'ah yale maregeo yaliiyotungwa kwa njia ya kuweka Shari'ah kikanuni (*taqneen tashri’ii*) kwa sababu ni dhihirisho miongoni mwa madhihirisho ya *taqleed* kwa kanuni za kimagharibi. Na kwa kuwa kuwekwa kanuni hizi hupelekwa na njia ya kufupisha *fiqhi* na huzidiwa na kuchukuliwa mas’ala ya *kifiqhi* yasiyo na dalili au dalili zake ni dhaifu. Na pia kuzidiwa na roho ya kuambatana na zama na tafsiri zilizo potoshwa ili ziafikiane na mtazamo wa kimagharibi katika kutatua matatizo. Pamoja na hayo ni kukosekana upande wa uwekaji Shari'ah (*tashri’*) na kukosekana ndani yake *ijtihadi*. Basi hazifai kutabikishwa na pia hazifai kufanywa maregeo, na kuwepo kwake imekuwa ni balaa kwa *fiqhi* na uwekaji Shari'ah kwa sababu ilikuwa ni majaribio ya kuigiza (wamagharibi) yaliyodhoofisha ujuzi wa watu katika *fiqhi* ya Kiislamu pamoja na kuwa utajiri uliopo katika fiqhi ya Kiislamu ni mwingi sana nao ni utajiri mkubwa wa kiShari'ah katika Ummah zote. Na ni dharura kwa makadhi na viongozi, lakini umewekwa kwa njia ya *kitaqleed* juu ya sura ya kikanuni wakaifupisha na kuiharibu. Ikawafanya makadhi kuwa ni wajinga katika *fiqhi* pindi walipo jitosheleza na ujuzi wa kanuni hizi. Isitoshe, ilikuwa imepoteza muundo wa kikanuni kwa sababu ilikuwa ni maelezo ya mkusanyiko wa dalili (*nusus*) za

*kifiqhi* za baadhi ya *mafuqaha* iliyopokelewa kwa idadi (*arqam*) zinazofuatana. Wala haikujaribiwa ndani yake kuweka *qai'da* jumla ambazo itakuwa ni maudhui ya mada na mas'ala tofauti kuwa chini yake. Bali imezifanya mas'ala yenyewe kuwa ndiyo ni mada na hii ndiyo isiyoafikiana pamoja na utangaji wa kikanuni, mpaka yale yaliyokuja katika baadhi ya mada katika qaida zimekuja kwa qaida zisizokuwa za kijumla na hazikuwa ila ni maarifa yaliyo nukuliwa kutoka vitabu vya *fiqhi*, na imekurubia kuwa zote ni katika jinsi hii. Kwa hayo haijuzu kuchukuliwa kanuni hizi wala kuchukuliwa kama maregeo kwa sababu ya kufisidika mbinu zake, uchache wa maalumuti zake na umbali wake na hukmu za kiShari'ah zinazo tambuliwa zilizo tegemea dalili fafanuzi.

Ili kuweka katiba na kanuni ili kudhamini *fiqhi* itakayofuatwa na makadhi na viongozi, ni lazima ipitie njia za kuweka Shari'ah zifuatazo:-

1. Ni lazima yasomwe matatizo ya mwanadamu na kuweka katiba jumla itakayo kuwa kwa umbo la *qaida* pana (*kuliyya*) zilizo jumla au hukmu za kiShari'ah za kijumla na ziwe zimetegemea fiqhi ya Kiislamu. Na ni lazima zichukuliwe ima kutokamana na rai ya *mujtahid* katika *mujtahidina* pamoja na kujua dalili zake na kukinaika nazo, au imma kutokamana na *Kitabu* na *Sunna* au *Ijma'a* ya Maswahaba au *qiyas* lakini kwa *ijtihadi* ya kiShari'ah hata kama ni *ijtihadi* ya kivipande nayo ni ijtihadi juu ya suala moja. Na ni lazima idokezwe sababu zilizowajibisha katika kila kifungu (cha katiba), *madhab* ambayo imeitegemea na dalili yake au kwa dalili ambayo amevua (*istinbat*) kutokamana nayo. Wala kattu isizingatie hali mbaya iliyoko mbele ya Waislamu wala hali ya Ummah nyinginezo wala nidhamu zisizokuwa za Kiislamu katika kuiandika (kuiweka) katiba.

2. Na ziwekwe hukmu za kiShari'ah (*mashari'*) kwa kanuni za kuadhibu waasi (*uqubaat*), haki (*huqooq*), ushahidi (*bayyinaat*) na nyinginezo juu ya msingi uliotangulia ikiambatana na katiba pamoja na kuashiriwa kwa *madhab* (iliyochukuliwa) na dalili, na iwe na matamshi ya kikanuni kwa misingi jumla ili iwe ni maregeo ya *kifiqhi* kwa makadhi na watawala.

3. Ziwe dalili (*nusus*) za kiShari'ah, fiqhi ya Kiislamu na elimu ya *usool ul-fiqhi* ndiyo maregeo katika kutafsiri katiba na kanuni kwa makadhi na watawala mpaka tuwasahilishie mbinu za ufahamu wa kindani.

Na haifai kwa kadhi kuhukumu kwa yale yaliokhalifu yaliyotabanniwa na serikali katika hukmu za kiShari'ah kwa sababu:

**أمرالإمام نافذ ظاهرا وباطنا**

**"Amri ya Imamu hutekelezwa kwa dhahiri na batini (siri)".**

Amma kwa yale yaliyomfikia kadhi yeye miongoni mwa kesi ambazo hakuna tabbani ya kihukmu kutoka kwa serikali, kadhi atahukumu kwa hukmu ya

kiShari'ah anayoiona yeye kuwa inaambatana na suala sawa sawa iwe ni rai ya mujtahid miongoni mwa mujtahidina au ni rai aliyoivua (istanbiti) mwenyewe kwa ijtihadi yake.

4. Pindi zinapovuliwa (*istinbat*) hukmu na zinapotabaniwa itiwe maanani ufahamu wa *waqi'ah* na kufahamu kinachohitajika katika kutatua tukio (*waqi'ah*) kutoka katika dalili za kiShari'ah nayo ni kufahamu hukmu ya Mwenyezi Mungu ambayo amehukumu nayo katika tukio (*waqi'ah*) hilo kisha hutabikishiwa hukmu juu ya waqiah. Na kwa maana nyengine ni kuunganisha ujuzi juu ya waqiah na kuifahamu pamoja na kujua hukmu ya Mwenyezi Mungu.

Serikali hutekeleza Shari'ah ya Kiislamu juu ya kila mwenye kubeba uraia wake sawa sawa awe ni Muislamu au asiyekuwa Muislamu. Amma wasiokuwa Waislamu huwachwa na wanayoitakidi na wanayoyaabudu. Husimamiwa katika mambo ya vilaji na vinywaji na mavazi kwa mujibu wa dini zao ndani ya nidhamu jumla. Mas'ala yao ya kibinafsi baina yao kama kwa mfano ndoa na talaka yataamuliwa kwa mujibu wa dini zao. Amma yaliyobakia katika mambo ya Shari'ah ya Kiislamu miongoni mwa maingiliano (*mu' amalat*), nidhamu za kuadhibu wahalifu, nidhamu za hukmu, uchumi na nyenginezo hizo hutekelezwa juu ya raia wote na kutekelezwa kwake sawa sawa ni juu ya Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Amma kwa Waislamu, serikali hutekeleza juu yao Shari'ah yote ya Kiislamu kutoka ibadati, akhlaqi, maingiliano, nidhamu ya kuadhibu wahalifu (na kadhalika). Na jukumu la serikali ni kutabikisha Uislamu kikamilifu na kuchukulia kutabikishwa kwake juu ya wasiokuwa Waislamu kama ulinganizi kwao kwa Uislamu. Kwa sababu Shari'ah ni jumla kwa wanadamu wote na hutabikishwa na serikali katika biladi yoyote inayoitawala kwa kubeba ulinganizi kwao kwa sababu siri ya mafanikio ya ukombozi wa Kiislamu huwa ni kubeba ulinganizi wa Kiislamu.

Uislamu una *aqeeda* (itikadi) inayo tokamana kwayo nidhamu, na nidhamu hizi ni hukmu za kiShari'ah zilizo vuliwa (*istinbat*) kutokana na dalili fafanuzi. Umebainisha Uislamu katika nidhamu zake jinsi ambavyo utakavyo tekeleza hukmu zake, kupitia hukmu za kiShari'ah. Na hukmu hizi za kiShari'ah ambazo hubainisha jinsi ya kutekeleza ndiyo twarika (*tariqa*) na zisizokuwa hizo huwa ni fikra na kufikia hapa huwa Uislamu ni *fikra* na *twarika*. Aqeeda na hukmu za kiShari'ah ambazo hutatua matatizo ya mwanadamu ndio *fikra* na hukmu za kiShari'ah ambazo hubainisha jinsi ya kutekeleza utatuzi huu, kuhifadhi *aqeeda* na kubeba ulinganizi ni *twarika*. Na kwa haya imekuwa twarika ya Kiislamu ni katika jinsi ya fikra yake na ni sehemu yake, basi haijuzu kubakia ulinganizi wa Uislamu juu ya kubainisha fikra yake bali ni wajibu ikusanye pia twarika. Na kupitia hayo umekuwa mfumo ni mkusanyiko wa *fikra* na *twarika*. Na imani juu ya *twarika* ni kama imani juu ya *fikra* basi imekuwa lazima iwe *twarika* pamoja na *fikra* kikamilifu bila ya kutenganishwa;

na ifungwe pamoja fungamano madhubuti kiasi ambacho haitumiwi kutabikishwa *fikra* ya Kiislamu ila kwa *twarika* ya Kiislamu na huwa mkusanyiko wake ni Uislamu ambao ndio unaotumika kuhukumu na hubebwa ulinganizi wake. Na maadamu *twarika* ipo katika Shari'ah basi ni wajibu ifungwe ndani yake na yaliyothubutu kiShari'ah na yaliyovuliwa (*istinbat*) kutokamana na dalili zake. Kama ilivyo thubutu katika Kitabu na Sunna hukmu za fikra hivyo hivyo ilithubutu ndani yake hukmu za twarika. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَإِمَّا تَخَافَنَّ مِنْ قَوْمٍ خِيَانَةً فَانْبِذْ إِلَيْهِمْ عَلَى سَوَاءٍ

**"*Na ukichelea khiyana kwa watu fulani basi watupilie ahadi yao kwa usawa.*"**

[Al-Anfal 8: 58]

Hii ni katika hukmu za twarika. Hivyo hivyo msemo wake (saw):

لاتتمنوا لقاء العدو وإذا لقيتموه فاصبروا

*"**Msitamani kukutana/kupambana na maadui na mnapo kutana/kupambana nao subirini**"* ni katika hukmu za twarika**.**

Hivyo hivyo hukmu zilizosalia za twarika kama zilivyo hukmu zengine huvuliwa kwa ijtihadi kutokamana na Kitabu, Sunna, *Ijma'a as-Sahaba* na *Qiyas*. Na ilipokuwa Sunna ndiyo yenye kuibainisha Kitabu, imekuwa fikra ni ya kijumla (*mujmal*) katika Kitabu (*Qur'an*) ikifafanuliwa katika Sunna. Na imekuwa twarika hivyo hivyo ni ya kijumla katika Qur'an iliyo fafanuliwa katika Sunna. Kwa hivyo imekuwa lazima kwetu kujaalia mwangaza (*nibras*) wa uongofu ni bwana wetu Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu na tuchukue hukmu za twarika kutokamana na vitendo vyake vinavyo patikana katika Sera yake, maneno yake na kunyamaza kwake kama tunavyo chukua kutokamana na Qur'ani kwa sababu yote hayo ni Shari'ah. Na tujaalie kiigizo chetu katika kuifahamu Sera, ni makhalifa walioongoka na masahaba waliosalia, na kufanya akili zetu ni chombo cha kivitendo (*fi'ala*) katika kufahamu na kuvua (hukmu) kwa mujibu wa mwelekeo wa kiShari'ah.

Na hukmu za ki-Sheria ambazo hubainisha jinsi ya utekelezaji hudokeza kwa vitendo. Hivyo basi hapana budi kutenda vitendo hivyo sawa sawa viwe miongoni mwake zinazo ambatana na utabikishaji au zinazo ambatana na ubebaji wa da'wah. Na vitendo hivyo sio mbinu (*wasila*) kwa sababu mbinu (*wasila*) ni kifaa kinachotumika wakati wa kutenda kitendo. Mbinu hizi hutofautishwa kwa kutofautika vitendo, hubadilika kwa mujibu ya dhurufu na huamuliwa na aina ya kitendo. Kwa hivyo hailazimiki ndani yake hali maalum.
Amma vitendo ambavyo hudokezwa na twarika hivyo havibadiliki bali hutendwa kwa mujibu ya dalili, wala haijuzu kutenda kitendo tofauti na kilichobainishwa na Shari'ah. Na wala hakitendwi kitendo nje ya mahala pake palipobainishwa na hukmu ya kiShari'ah.

Uchunguzi katika vitendo hivi ambavyo vimedokezwa na hukmu za kiShari'ah vinavyo ambatana na twarika yabainika kuwa vitendo hivyo ni vya kimada vilivyo na natija ya kushikika na sio vitendo vinavyo hakikisha natija isiyoshikika hata kama aina hizi mbili za vitendo huhakikisha thamani moja. Mfano dua ni kitendo kinacho hakikisha thamani ya kiroho na jihadi ni kitendo cha kimada kinacho hakikisha thamani ya kiroho, lakini dua hata kama ni kitendo cha kimada lakini huhakikisha natija isiyoshikika nayo ni thawabu hata kama kusudio la mwenye kuomba dua ni kuhakikisha thamani ya kiroho. Kinyume na jihadi ambayo ni kupigana na maadui nacho ni kitendo cha kimada kinacho hakikisha natija ya kushikika nayo ni kukomboa ngome au mji au kumuua adui na yanayo fanana na hayo, hata kama makusudio ya mujahid ni kuhakikisha thamani ya kiroho. Na kufikia hapa huwa vitendo vya *kitwarika* ni vitendo vya kimada vinavyo hakikisha natija ya kushikika na hukhtalifiana na vitendo vinginevyo. Kwa hivyo haichukuliwi dua kama *twarika* ya jihadi hata kama *mujahid* humuomba Mwenyezi Mungu, hivyo hivyo haichukuliwi mawaidha kama *twarika* ya kumzuia mwizi hata kama hupewa mawaidha na huelekezwa (huongozwa). Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّى لاَ تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الدِّينُ لِلَّهِ

**"*Piganeni nawo mpaka pasiwepo fitina na Dini iwe ya* Mwenyezi Mungu tu."** [Al-Baqarah 2: 193]

Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا

**"*Mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao*"**
[Al-Ma'idah 5:38]

Kwa hivyo haikubaliki kikamilifu kwamba vitendo vinavyotumika kutabikisha/ kutekeleza fikra ya Uislamu kwamba ni vitendo visivyo hakikisha natija ya kushikika na huhisabiwa hilo kuwa ni kinyume na twarika ya Kiislamu. Na wala hakuna tofauti baina ya vitendo ambavyo hutumiwa kutekeleza hukmu zinazo ambatana na utatuzi wa matatizo na baina ya vitendo ambavyo hutumiwa kubeba da'wah ya Kiislamu. Mfano *swala* huchukuliwa ni katika fikra, na twarika ya kuitekeleza ni serikali. Basi haijuzu serikali kutumia mafundisho na muongozo tu kuwa ndio njia (*twarika*) ya watu kusimamisha swala bali ni wajibu kuadhibu mwenya kuacha swala adhabu ya kimada kama kwa mfano jela na hata kama serikali itasimama kufundisha na kuongoza. Na mfano wa hilo pia ni ubebaji wa da'wah ya Kiislamu ambayo ni fikra, na twarika ya kuitekeleza kupitia serikali ni jihadi yaani kupigana vita na maadui. Basi haijuzu kutumiwa masomo ya *Sahihi ya Al-Bukhari* kuondosha vizuizi vya kimada vilivyo mbele ya da’wah bali hapana budi kutumia jihadi nayo ni kupigana na maadui mapigano ya kimada. Na hivyo ndivyo (hutekelezwa) vitendo vyote vya kitwarika.

Ni lazima ijulikane kuwa hata kama kitendo ambacho hudokezewa na twarika ni kitendo cha kimada kilicho na natija ya kushikika lakini hapana budi kupelekwa kitendo hicho kwa maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu kwa lengo la kunali (kupata/kutafuta) radhi za Mwenyezi Mungu. Kama vile hapana budi imtawale Muislamu kudiriki kwake fungamano lake na Mwenyezi Mungu (swt) basi atajikurubisha kwa (Mwenyezi Mungu) kwa swala, dua, kusoma Qur'an na mfano wake. Ni lazima aitakidi Muislamu kuwa *nusra* (ushindi) hutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo hapana budi iweko *taqwa* (uchajimungu) iliyokita katika vifua ili kutabikisha hukmu za Mwenyezi Mungu. Na hapana budi kuomba dua na hapana budi kudumisha fungamano na Mwenyezi Mungu pindi vinapotendwa vitendo vyote.

Huu ni katika upande wa *twarika* na kuwa ni hukmu za kiShari'ah ambazo ni wajibu tujilazimishe nazo wala tusizikhalifu, na katika upande wa vitendo kuwa ni vitendo vinavyo hakikisha natija ya kushikika. Amma kwa upande wa kufikia natija ni lazima ifuatwe qaida ya kivitendo, nayo ni kuwa kitendo hujengwa juu ya *fikra* na huwa kwa ajili ya lengo maalum. Hii ni kwa sababu kule kuhisi kwa tukio (*waqi'ah*) ikiambatanishwa pamoja na elimu iliyotangulia ni lazima izae fikra. Ni lazima iungane *fikra* hii na kitendo na iwe fikra na kitendo ni kwa ajili ya lengo maalumu, na yote hayo yajengwe juu ya imani mpaka abakie mwanadamu daima katika mwenendo ndani ya mazingara ya kiimani. Wala haijuzu katu kutenganisha kitendo na *fikra* au na lengo maalum au imani; katika utengamano huu, jinsi utakavyo kuwa kidogo, ni hatari kwa kitendo chenyewe, kwa natija yake na kwa kudumu kwake. Kwa hivyo hapana budi lengo maalum liwe ni lengo la kufahamika lililowazi kwa kila mwenye kutaka kutenda kitendo kabla ya kutekeleza kitendo. Na ni lazima iwe mantiki ya hisia ndiyo iwe msingi, yaani iwe fahamu na kufikiria ni zenye kutokamana na hisia wala sio mujarad ya mawazo juu ya qadhiya za kindoto. Na iwe hisia kwa *waqi'ah* ndiyo inayoathiri ubongo na pamoja na kuwepo elimu iliyotangulia kuleta harakati za kibongo ambazo ndiyo fikra. Na hii ndiyo inayohakikisha undani katika kufikiria na natija/mazao yake katika kitendo. Na mantiki ya hisia hupelekea kwa hisia ya kifikra yaani kwa hisia ambayo hutilia nguvu fikra kwa mwanadamu. Kwa haya huwa kwa mfano hisia ya wabebaji da'wah baada ameifahamu ina nguvu kuliko hisia kabla hapo.

Ni hatari kwa wanadamu kuruka kutoka kwa hisia mpaka kitendo bila ya kupitia fikra. Hali hii hii haibadilishi hali ilivyo (*waqi'ah*). Bali humfanya mwanadamu ni mwenye kufuata mambo yalivyo na kuyaitikia: humpelekea kwa ufahamu ulio didimia/zorota na hufanya hali ilivyo (*waqi’ah*) kuwa ni chimbuko la fikra wala sio mahala pa kufikiriwa. Basi hapana budi kwa hisia kwanza kupelekea katika fikra, kisha fikra hii ifikishe kwa kitendo. Na hii ndiyo huwezesha mwanadamu kunyanyuka (kupanda juu) kutoka hali ilivyo (*waqi’ah*) na huwezesha juhudi za kugura kuelekea hali nzuri kwa kugura

kimapinduzi. Yeyote yule anayetenda kwa msingi wa hisia pekee, hatobadilisha hali ilivyo (*waqi'ah*) bali hutenda kwa kuambatanisha nafsi yake na hali ilivyo na hubakia nyuma na mwenye kuzorota. Na yule ambaye huhisi hali ilivyo kisha akafikiria jinsi ya kuibadilisha kisha akatenda kwa mujibu ya fikra hii, huyu ndiye anayebadilisha hali ilivyo kwa mujibu wa mfumo wake na hubadilisha mabadiliko ya kijumla. Huyu ndiye anayeafikiana na twarika ya kimapinduzi ambayo ndiyo twarika ya kipekee ya kuregesha maisha ya Kiislamu. Hii ni kwa sababu njia hii hulazimisha kuwa fikra iwe ni natija ya hisia na iwe wazi fikra hii kiasi ambacho itachora ramani ya kiufundi kwa kuifahamu vizuri *fikra* na *twarika*. Basi mwanadamu hufahamu mfumo ufahamu uliosahihi utakaompeleka kwa kutenda vitendo mpaka iwe fikra imezalisha ndani yake mapinduzi ya kijumla. Basi wakati huo huendelea mbele mwanadamu katika kuandaa watu, mujtama na mazingira kwa fikra hii ili izalishe mapinduzi katika rai jumla (*rai' 'amm*) baada ya kupatikana busara ya ufahamu jumla (*wai' amm*) juu ya mfumo wake kwa *fikra* na *twarika*. Kwa msingi huu pamoja na uongozi hutabikishwa mfumo utabikishaji wa kimapinduzi bila kukubali kutabikisha kidogo kidogo (*tadarruj*) au kuweka viraka. Na njia hii ya kimapinduzi hulazimisha fikra iwe ni natija ya hisia na iunganishwe (*fikra*) na kitendo kwa ajili ya lengo maalum. Wala hakuna itakayo fikia hapa ila fikra ya kindani.

Na fikra hii ya kindani yahitaji mwenye kuileta au kuikuza na kuifanya kama ardhi yenye rutuba (*khasaba*). Na njia ya kimapinduzi huhitaji kuwaandaa watu kwa mfumo wa Kiislamu na kuandaa mujtama nao. Na kuileta fikra hiyo ya kindani na kuandaa watu kimfumo hulazimisha wale wanaotaka kuleta mageuzi kuusoma Uislamu na hivyo hivyo hulazimisha kuusoma mujtama na hayapatikani hayo ila kwa njia ya kuikuza akili kwa maalumati. Masomo ni njia sahali na ya karibu ya kufikisha maalumati hizi kwa akili ili isaidie katika kuzalisha fikra.

Uislamu una njia makhsusi katika kuusoma. Kuifuatilia (njia hii pekee) ndiyo inayozalisha athari kwa masomo haya. Njia hiyo hulazimisha kusoma maalumati ili kuyatekeleza, na mwenye kuyapokea mafundisho hayo mapokezi ya kifikra yanayo athiri miondoko yao. Hii huathiri hisia mpaka iwe hisia yake juu ya uhai na majukumu yake ni hisia ambayo ni natija ya fikra inayo athiri, mpaka ipatikane katika nafsi ya mwenye kusoma (Uislamu) moto, hamasa, fikra na maarifa mengi kwa wakati mmoja na huwa utabikishaji ni natija ya kikawaida. Na njia hiyo ya masomo, huleta ufahamu kwa mwenye kusoma na kuleta ndani yake uweza wa kuwasilisha aliyo yafahamu kwa sura ya kuathiri. Hakika yake hupanua fikra na huunganisha fikra na hisia na humfundisha mwenye kusoma uhakika/maalumati ambayo huyatumia kutatua matatizo maishani. Kwa haya ni lazima yaepukane mafunzo kuwa tu ni mujarad wa elimu tu, mpaka asiwe mwenye kusoma kuwa ni kitabu chenye kutembea. Mafunzo haya pia yasiwe ni mujarad wa mawaidha na miongozo

ama itakuwa ya juu juu (*sathiya*) pasina joto la imani. Na ni lazima isichukuliwe mafundisho ya Kiislamu kuwa ni mafunzo ya mujarad ya kielimu na mawaidha. Bali kuchukuliwa kwake kuwa ni elimu na mawaidha huwa ni hatari kwa kazi ya ulinganizi (*da'wah*) na huitatiza na kuilemaza kwake.

Ili kufikia lengo ambalo kwa ajili yake kitendo hutendwa, ni lazima ifahamike kuwa kulifikia lengo hili huhitaji kujitolea na kuipa umuhimu, na kujifunga na majukumu yaliyo lazimishwa na jukumu la kichama juu ya majukumu ya Uislamu. Na Uislamu una majukumu: (yenye) kukanya (*salibiyya*) na yenye kuamrisha (*ijabiyya*) yanayo kukalifisha kimali, kiwiliwili na kinafsi. Na miongoni mwa majukumu haya ni taklifu za faradhi na wajibu kwa kila mmoja, na miongoni mwake ni yale yaliyo juu ya faradhi na wajibu yanayo tendwa kwa khiyari na wale walio na mustawa wa juu wa kiroho na wa kiakili, nao ni wale ambao wanataka kuzidi kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu (swt). Na kutenda haya majukumu hulazimu kufikia lengo. Kwa hivyo ni lazima kila mmoja kujisukuma na kuilazimisha nafsi kutenda majukumu ya faradhi kwa kila upande: kimali, kiwiliwili na kinafsi mpaka ipatikane matarajio ya kufikia lengo.

Ili kitendo kuzaa natija, hapana budi kufafanua mahali ambapo kitendo hicho huanzia na kikundi ambacho huanzia kukitendea nacho. Hakika Uislamu ni wa kiulimwengu nao huwatazama wanadamu wote na huwachukulia wanadamu wote kuwa ni sawa. Katika ulinganizi Uislamu hauupi uzito wowote tofauti ya kimazingira, hali, mahala, na yanayo fanana na hayo. Bali huwachukulia wanadamu wote kuwa wanafaa kupokea ulinganizi na huwachukulia Waislamu ndiyo wanaohusika na kubalighisha ulinganizi huu kwa wanadamu wote. Lakini pamoja na hayo ulinganizi wa Kiislamu hauanzi kiulimwengu kwa sababu lau kuanza nayo (kiulimwengu) huchukuliwa ni kitendo kinachofifia wala hakifikishi kata kata kwa natija yoyote. Bali hapana budi kuwa uanze kwa mtu binafsi na mwisho iwe ni kwa ulimwengu. Kwa hivyo ni wajibu kubebwa ulinganizi katika mahali ambapo itamakinika ndani yake mpaka iwe ni nukta ya kianzio kisha huchukuliwa hapa au mahali pengine ambapo itamakinika ndani yake ulinganizi kuchukuliwa ni nukta ya kugura inayogura kutokamana nayo ulinganizi katika njia yake. Kisha huchukuliwa hapo au kwengineko kuwa ni nukta ya kumakinika inayosimama ndani yake serikali, kisha serikali humakinisha da'wah katika mahali hapa na kisha (da'wah) ikaendelea katika njia yake ya kimaumbile: Njia ya jihadi. Lakini hata kama mahali huchukuliwa kama mahala pa kitendo katika kila nukta, isipokuwa kile ambacho hugura kutoka nukta moja mpaka nukta nyingine ni ulinganizi sio mahali na hugura ulinganizi katika mahala pote ambapo hutendwa ndani yake katika wakati mmoja. Na hakika yake, hata kama ni lazima kulengwa mahali ambapo patakuwa ni nukta ya kianzio kisha kuwepo nukta ya kugura na nukta ya kumakinika, isipokuwa kulengwa mahali katika kila nukta miongoni mwa nukta hizi tatu sio katika mzunguko ambao

mwanadamu huutawala juu yake kwa sababu yeye hana elimu juu ya hilo, bali jambo hili huingia katika mzunguko unaomtawala mwanadamu. Wala si juu ya mwanadamu ila kujipeleka kutenda vitendo ambavyo huingia ndani ya mzunguko anao utawala juu yake; amma vitendo ambavyo ni katika mzunguko mwengine hutokea kwa mujibu ya matakwa ya Mwenyezi Mungu na *qadhaa* Yake.

Amma kuchaguliwa nukta ya kianzio huwa hakika ni katika mahali ambapo hupatikana ndani yake yule aliyenawiri katika fahamu zake, mwanga wa mwanzo wa ulinganizi na Mwenyezi Mungu humtayarisha kwa kubeba ulinganizi huo. Waweza kuhisi watu tofauti tofauti kwa hisia hiyo lakini yule ambaye Mwenyezi Mungu amemtayarisha kubeba ulinganizi hajulikani mpaka atakapotokea na aanze ulinganizi katika mahala ambapo yeye huishi ndani yake. Na huwa mahala hapo ni nukta ya kianzio.

Amma nukta ya kugura, hakika yake hutegemea kuwa tayari kwa mujtama, kwa sababu mujtama hutofautiana katika fikra, hisia na nidhamu. Basi mahala ambapo huwa mujtama wake ni mzuri na mazingara mazuri juu ya fikra mpya huwa ni nukta ya kugura. Ni aghlabu sana sana kuwa mahali ambapo ni nukta ya kianzio kuwa ndio nukta ya kugura hata kama hilo sio dharura kwa sababu mahala panapo stahiki kugura ni mahala ambapo hukithiri ndani yake dhuluma za kisiasa na za kiuchumi na huvuka mipaka katika kumkanusha Mwenyezi Mungu na ufisadi.

Amma nukta ya kumakinika, hii hutegemea kufaulu kwa ulinganizi katika mujtama maalum. Hivyo basi mahali popote ambapo ulinganizi hauathiri mujtama wake wala hauwezi kujiwekea mazingira yake hauwezi chukuliwa kuwa ni nukta ya kumakinika licha watakavyo kuwa wengi idadi ya wabebaji mfumo. Na mahali ambapo ndani yake fikra na twarika hubebwa na mujtama na kuenea mazingara hufaa kuwa ni nukta ya kumakinika vyovyote itakavyo kuwa idadi ya wabebaji mfumo.

Kwa hivyo haijuzu kwa wabebaji ulinganizi kupima ulinganizi kwa idadi ya wabebaji wake. Kipimo hicho ni cha makosa wazi na ni hatari kwa ulinganizi kwa sababu hubadilisha ubebaji ulinganizi kutoka mujtama mpaka kwa watu binafsi na hili husababisha kuchelewa na pia huenda likasababisha kuzorota katika mahali hapo. Na siri ya hilo ni kuwa mujtama haukubuniwa juu ya watu binafsi kama wanavyo waza watu wengi. Bali watu ni sehemu katika kundi (jamii), na kinacho unganisha baina ya watu hao katika mujtama na vipengee vyengine kama fikra, hisia na nidhamu. Kwa hivyo hutumiwa ulinganizi kusahihisha fikra, hisia na nidhamu, na ulinganizi huu wa kikundi ni ulinganizi kwa mujtama sio kwa watu binafsi. Na kubadilisha watu binafsi haiwi ila wawe viungo katika kikundi ya kijumuiya kinachobeba ulinganizi kwa mujtama. Kwa hivyo wabebaji ulinganizi wanaofahamu uhakika wake hutegemea juu ya

mujtama kubeba ulinganizi kwake. Huchukulia kuwa kutengenea mtu binafsi haifikishi kutengenea kwa mujtama. Bali haidhamini kutengenea yeye kutengenea kulio kwa daima. Bali huwa hutengenea mtu binafsi kwa kutengenea mujtama, na pindi inapotengenea mujtama hutengenea mtu binafsi. Kwa hivyo ni wajibu ielekezwe ulinganizi wao kwa mujtama, kwa kufuata qaida:

**إصلح المجتمع يصلح الفرد ويستمر إصلاحه**

***"Tengeneza mujtama na itapelekea kutengenea kwa mtu binafsi"***

Kwa kuwa mujtama hufanana na maji katika birika kubwa, pindi yanapowekwa chini au pambizoni mwake kile kinachosababisha ubaridi hubaridika maji na hugeuka kuwa barafu. Hivyo hivyo yanapowekwa katika mujtama misingi fisadi huwa (mujtama) katika ufisadi na hubakia katika kuzorota na kufifia. Pindi kunapowekwa ndani yake (mujtama) misingi inayo gongana hudhihirika katika mujtama mgongano na hubakia mujtama ukikorogeka katika mgongano na kukosa utulivu. Na pindi kunapowekwa chini ya birika moto unaochemsha, maji hushika moto kisha hutokota na huwa mvuke unaosukuma unaharikisha. Hivyo hivyo ikiwekwa katika mujtama mfumo sahihi huwa ni mwasho katika mujtama inayobadilika kwa moto wake mpaka kutokota, kisha huwa ni nguvu ya msukumo. Na hutabikishwa mfumo na kubebwa ulinganizi wake kwa mujtama nyingine. Na hakika hata kama kubadilika mujtama kutoka hali moja hadi nyingine inayogongana au, kwa matamshi mengine, kupinduka kwake (mujtma) kutoka hali moja hadi nyingine haishuhudiwi kama isivyo shuhudiwa kubadilika maji katika birika, lakini wajuzi wa mujtama wanaoamini kuwa mfumo wanaoubeba ni moto na nuru unaochoma na kuangaza hujua kuwa mujtamaa uko katika hali ya kubadilika na kuwa itafikia katika daraja ya kuchemka kisha itafikia katika daraja ya *haraka* (matendo) na msukumo. Kwa hivyo hutilia maanani kwa mujtama (wala si kwa mtu binafsi).

Kwa hayo, hakika mahali ambapo panastahiki kuwa ni pa kumakinisha hapajulikani kwa sababu hutegemea kwa kuandaliwa (kuwa tayari) mujtama si tu juu ya nguvu ya ulinganizi. Hakika ya ulinganizi wa Kiislamu Makka ulikuwa na nguvu na pamoja na hilo Makka hata kama ilikuwa ni nukta ya kianzio chake na kustahiki kuwa ni nukta ya kugura na ikagura kutoka kwake ulinganizi, lakini haikustahiki kuwa ni nukta ya kumakinika bali nukta ya kumakinika ilikuwa ni Madina. Kwa hivyo aliguria Mtume (saw) baada ya roho yake kutua na mutjama wake (mujtamaa wa Madina). Akasimamisha utawala Madina ambao kutokamana nao ililingania kwa nguvu kwa maeneo mengine yaliyobakia ya pembe za bara Arabu na kisha kwa dunia yote.

Na kufikia hapa, twaweza kusema kuwa wabebaji ulinganizi haimkiniki kwao wao kujua mahali ambapo hustahiki kuwa nukta ya kugura wala mahali ambapo hustahiki kuwa nukta ya kumakinika, wala haimkiniki kwao wao kujua

vyovyote watakavyo kuwa mahadori na udadisi bali elimu ya hilo iko kwa Mwenyezi Mungu (swt). Kwa hivyo ni wajibu kuwa mategemeo ya wabebaji ulinganizi yawe kwa kitu kimoja nayo ni imani kwa Mwenyezi Mungu (swt) na iwe vitendo vyao vyote visimame tu juu ya imani hii sio juu ya chengine. Na kwa imani juu ya Mwenyezi Mungu sio kwa mwengine hufaulu ulinganizi.

Imani juu ya Mwenyezi Mungu hulazimisha ukweli wa kumtegemea (*tawakal*) Yeye, na kutaka msaada kutoka Kwake kwa sababu Yeye pekee ndiye anayejua siri na yaliyofichikana, na Yeye ndiye anayewapa taufiq (ushindi/kuwaafiki) wabebaji ulinganizi na kuwaongoza njia ya sawa na njia ya uongofu. Kwa hivyo hapana budi kuwa na nguvu ya imani na hapana budi na ukamilifu wa kumtegemea (tawakal) Mwenyezi Mungu na kudumu kutaka msaada kutoka Kwake Mwenyezi Mungu (swt). Na imani humlazimisha muumini kuamini mfumo yaani imani kwa Uislamu kwa sababu hutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt) na hulazimu iwe imani iliyokita iliyothibiti isiyokuwa na shaka, wala hakuna uwezekano wa kupenya shaka. Kwa sababu kila hatari ya shaka ndogo katika mfumo hupelekea kwa uzorotefu. Bali huenda likapelekea katika ukafiri na uasi (twajilinda na Mwenyezi Mungu kwa hayo).

Imani hii iliyo na nguvu ambayo isiyopenya kwake shaka ni jambo la lazima kwa wabebaji ulinganizi kwa sababu ndiyo inayodhamini kudumu mwenendo wa ulinganizi kwa njia ya haraka, pana (kuelekea) katika njia iliyonyoka. Na imani hii huwajibisha ulinganizi uwe wazi unaopambana na kila kitu; utapambana na ada na desturi, fikra za kimakosa, ufahamu uliofisidika, utapambana hata na rai jumla ikiwa ni ya kimakosa hata kama itazuiliwa katika kupambana nayo. Itapambana na itikadi na dini za uongo hata kama itakabiliana na balaa za wafuasi wake. Kwa hivyo hutofautika ulinganizi uliojengwa juu ya msingi wa aqeeda ya Kiislamu kwa uwazi, ushujaa na nguvu, na fikra na hupambana na kila anaye khalifu fikra na twarika yake na kukabiliana naye ili kubainisha ubovu wake bila kujali natija yake na matokeo yake, na bila kujali aghlabu ya Ummah utaafikiana au wataukataa na kuupinga. Kwa hivyo mbebaji ulinganizi hawasifu kwa kuvuka mipaka watu wala kuwapaka mafuta. Hawanyenyekei wale wanaomiliki uzito katika mujtama miongoni mwa viongozi na wengine wala hawaonyeshi urafiki bali hushikamana kwa mfumo peke yake bila kuingia katika hisabu ya kitu chochote kisichokuwa mfumo.

Imani hii pia huwajibisha ubwana uwe kwa mfumo pekee yaani Uislamu pekee na kuchukuliwa mifumo mingine kuwa ni ukafiri jinsi itatakavyo tofautika na kukhtalifiana mifumo hiyo:

إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الإِسْلاَمُ

***"Hakika dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu."*** [Aal-e-Imran 3: 19]

Kila asiyeamini Uislamu ni kafiri katika mtazamo wa Kiislamu kwa hivyo haijuzu kata kata kwa mbebaji ulinganizi wa Kiislamu kuwaambia wanaobeba usiokuwa Uislamu sawa sawa ikiwa ni dini au mfumo: '***Shikamaneni na mfumo wenu na dini yenu***' bali ni wajibu awalinganie kwa Uislamu kwa hikma na dalili za kiakili ili wasilimu kwa sababu ulinganizi hulazimu wabebaji wake wafanye kazi ili ubwana uwe kwa Uislamu peke. Na sio maana ya kuwawacha wasiokuwa Waislamu na dini yao na wanayo yaitakidi kuwa ni kukiri dini zao bali ni kuitikia amri ya Mwenyezi Mungu ambao amewajibisha kutolazimisha watu kuukubali Uislamu kwa nguvu na akawajibisha kuwawacha watu na itikadi zao, dini zao na ibada zao maadamu itabakia kibinafsi sio kijumla na wasiwe na umbo (*kiyan*) ndani ya utawala wa Uislamu. Kwa hivyo Uisilamu hukataza kuwepo vyama au makundi ya kisiasa yasiyokuwa ya Kiislamu yanayosimama juu ya msingi unaogongana na Uislamu, na huruhusu vyama na makundi yaliyo ndani ya mipaka ya Uislamu. Hivi ndivyo inavyolazimu imani juu ya mfumo wa Kiisilamu kuwa bwana/juu ya mujtama wala kutoshirikiana pamoja na yeyote asiyekuwa wao.

Imani kwa Uislamu ni tofauti na kufahamu hukmu na Shari'ah yake kwa sababu imani juu yake imethubutu kwa njia ya akili kwa hivyo haipenyi ndani yake shaka. Amma kufahamu hukmu zake, hilo halitegemei akili peke yake bali hutegemea juu ya kujua lugha ya kiarabu, uweza wa kuvua hukmu *(istinbat)* na kuzijua hadithi sahihi kutoka katika hadithi dhaifu. Kwa hivyo imekuwa juu ya wabebaji ulinganizi ***kuchukua fahamu zao (juu ya hukmu) kuwa ni za sawa zilizo na uwezekano wa makosa na fahamu za wengineo kuwa ni za kimakosa zilizo na uwezekano wa kupata*** mpaka iwezekane kwao kuulingania Uislamu na ahkamu zake kwa mujibu wa fahamu na *istinbat* zao, na waweze kubadilisha fahamu za wengineo ambazo wanazichukulia kuwa ni za kimakosa zilizo na uwezekano wa kupata kwa fahamu zao wanazo zichukulia kuwa ni za sawa zilizo na uwezekano wa kukosa. Kwa hivyo haisihi kwa wabebaji ulinganizi kusema juu ya ufahamu wao kuwa '*hino ni rai ya Uislamu*' bali ni juu yao kusema juu ya rai yao kuwa '*hino ni rai ya Kiislamu*.' Walikuwa watu wa madhab miongoni mwa mujtahidina wakichukulia *istinbat* zao kwa ahkamu kuwa ni sawa inayobeba uwezekano wa kukosa, na kila mmoja wao alikuwa akisema

**إذا صح الحديث فهو مذهبي واضربوا بقولي عرض الحائط**

***"Inapokuwa sahihi hadithi basi hiyo ndiyo madhab yangu na iwacheni rai yangu"***

Hivyo hivyo ni wajibu kwa wabebaji ulinganizi kuchukulia rai zao ambazo wamezi tabanni au kuzifikia kutokana na Uislamu kwa kuchukua fahamu zao ni rai za kisawa zinazobeba uwezekano wa kukosa lakini imani yao kwa Uislamu kama aqeeda (itikadi) haijuzu kupenya ndani yake shaka yoyote. Bali huchukua wabebaji ulinganizi fahamu zao kwa kuchukua huko kwa sababu ulinganizi umepanda katika nafsi zao hamu ya kutaka ukamilifu, na

huwalazimisha daima kuchunguza uhakika na daima kuchunguza kila wanalolijua na kulifahamu mpaka waisafishe kutoka kila kigeni ambacho huenda kime gandamana nacho, na kuweka mbali kila kinacho jikurubisha nacho kwa uwezekano wa kujiunga nayo na kuchukuliwa kuwa ni sehemu yake. Hilo ni kuhakikisha kwamba ufahamu wao ubakie ni sahihi na fikra ya kindani, na mpaka ibakie fikra ni nyeupe na safi. Kwa sababu kwa kadri ya usafi wa fikra na uweupe wake huwawezesha kusimamia ulinganizi. Kwa sababu usafi wa fikra na uwazi wa twarika ndiyo dhamana ya kipekee ya kufaulu na kuendelea kwa da'wah.

Isipokuwa uchunguzi (*tanqib*) huu juu ya uhakika wa kutafuta la usawa haimaanishi kuwa fahamu zao sio thabiti bali ni lazima iwe thabiti kwa sababu imetokamana na fikra ya kindani, ambayo imethubutu kuliko fahamu yoyote isiyokuwa hiyo. Kwa hivyo imekuwa juu ya wabebaji ulinganizi kuwa macho kuwa ulinganizi wao ni katika ufahamu wao kwanza, wakitahadhari kufitiniwa na wengineo kwa ulinganizi wao, na fitina hii ni hatari iliyo mbaya kwa ulinganizi, kwa hiyo Mwenyezi Mungu alimhadharisha nayo Mtume wake (saw):

وَاحْذَرْهُمْ أَنْ يَفْتِنُوكَ عَنْ بَعْضِ مَا أَنزَلَ اللَّهُ إِلَيْكَ

“***Nawe tahadhari nao wasije kukufitini ukaachabaadhi ya aliyo kuteremshia Mwenyezi Mungu.***” [Al-Ma'idah 5: 49].

Imeripotiwa kwamba Umar (ra) alimwambia kadhi wake Shuraih pindi alipokuwa akimuusia kutizama katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu, akamwambia

**“watu wasikupotoshe kutokamana nacho.”**

Kwa hivyo ni lazima watahadhari wabebaji ulinganizi kutoka tamko ambalo lagongana na Uislamu hata kama litatoka kwa mtu mwenye ikhlasi au rai yoyote ambayo huenda akaiona mwenye pupa kwa ulinganizi na kuisukuma (kuitilia nguvu) kwa hoja ya maslahi na ilhali ina khalifu Uislamu. Basi watahadhari nayo wala wasikubali hilo kutokamana na yeyote, kwa sababu katika hayo kuna upotevu uliowazi. Ni lazima ulinganizi kutofautisha baina **ulinganizi wa Uislamu** na ulinganizi wa **kurudisha Uislamu maishani** na pia ni lazima kutofautisha baina **ulinganizi wa kundi katika Ummah** kama kikundi cha Uislamu na baina ya **ulinganizi unaobebwa na serikali ya Kiislamu**.

Amma kutofautisha baina ya ulinganizi wa Uislamu na ulinganizi wa kurudisha Uislamu maishani, huwa ni katika kufafanua lengo ambalo ulinganizi inajipeleka kwalo. Na tofauti baina yake ni kuwa hubebwa ulinganizi wa Uislamu kwa wasiokuwa Waislamu na hulinganiwa ili waukubali na kuingia ndani yake na hawa huwa njia ya kivitendo ya kuwalingania ni kuhukumiwa na Uislamu kupitia serikali ya Kiislamu mpaka waone nuru ya Uislamu; na

hulinganiwa wa Uislamu katika kubainisha aqeeda (itikadi) yake na hukmu zake mpaka watambue ukubwa wa Uislamu. Kwa hivyo imekuwa ni lazima serikali ya Kiislamu kubeba ulinganizi wa Uislamu.

Amma ulinganizi wa kurudisha maisha ya Kiislamu ni lazima ubebwe na kikundi wala si watu binafsi. Na ulinganizi huu wa kurudisha maisha ya Kiislamu utazamwe kama ifuatavyo: Mujtama ambao huwa watu wake kwa jumla yao ni Waislamu na huhukumiwa na yasiyokuwa Uislamu, huwa ni mujtama usiokuwa wa Kiislamu na husimama juu yake kuwa ni *Dar ul-Kufr.* Na hulinganiwa ndani yake ili isimame serikali ya Kiislamu itakayo tabikisha/tekeleza Uislamu ndani yake na kubeba ulinganizi wake kwa wengineo. Hili ikiwa hakuna serikali ya Kiislamu. Ikiwa kuna serikali ya Kiislamu inayotabikisha Uislamu kikamilifu hulinganiwa mujtamaa wake ili iwe eneo (*wilaya*) katika eneo (*wilaya*) la serikali ya Kiislamu ili ihukumiwe kwa Uislamu na ili iwe ni sehemu yake. Hubebwa ulinganizi wa Kiislamu mpaka iwe mujtama wa Kiislamu na itakuwa kweli wakati huo kuwa ni *Dar ul-Islam*. Kwa sababu haijuzu kwa Muislamu kuishi katika *Dar ul-Kufr* bali ni juu yake pindi inapokuwepo *Dar ul-Islam* na ilhali yeye yuwaishi katika *Dar ul-Kufr* kufanya kazi ili aifanye kuwa ni Dar ul-Islam au agurie *Dar ul-Islam.*

Amma kutofautisha baina ulinganizi unaobebwa na kikundi katika Ummah wa Kiislamu na baina ya ulinganizi unaobebwa na serikali ya Kiislamu, hili ni muhimu ili kujua aina ya vitendo ambavyo hutekelezwa na wabebaji ulinganizi. Na tofauti baina yake ni kuwa ulinganizi unaobebwa na serikali ya Kiislamu husimama kivitendo pale serikali inapotabikisha Uislamu kwa ndani utabikishaji kamilifu na kijumla mpaka Waislamu wanapate kufaulu (*sa'ada*) maishani na waone wasiokuwa Waislamu wanaoishi ndani ya utawala wa serikali ya Kiislamu nuru ya Uislamu, basi wataingia wenyewe kwa khiyari zao wakiwa wameridhia na majasiri. Serikali itabeba ulinganizi wa kiinje, si tu kwa njia ya matangazo na kusherehesha hukmu za Kiislamu bali kwa kuandaa nguvu kwa jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, kwa ajili ya kuzitawala biladi jirani kupitia Uislamu. Kuzitawala kwa Uislamu ndiyo njia ambayo aliyoitumia Mtume (saw) na pia ilitumiwa na Makhalifa wake baada yake mpaka serikali ya mwisho ya Kiislamu. Kwa hivyo imekuwa kubebwa ulinganizi na serikali ndiyo upande wa kivitendo katika ulinganizi wa kindani na kinje.

Amma ulinganizi ambao hubebwa na kundi au kikundi, hivyo ni vitendo vinavyo ambatana na fikra wala haviambatani na kutenda vitendo vyenginevyo. Kwa hivyo huchukuliwa upande wa kifikra sio upande wa kivitendo. Itasimama kwa kikundi yaliyo faradhishwa juu yake na Shari'ah katika mfano wa hali hiyo (ya kifikra), mpaka ipatikane serikali ya Kiislamu kisha ianze upande wa kivitendo katika serikali. Na hayo ni pamoja na kuwa ulinganizi huelekezwa kwa Waislamu, waufahamu Uislamu ili warudishe

maisha ya Kiislamu, na kupambana na kila anaye simama mbele ya ulinganizi huu kwa mbinu ambayo inayowajibisha mapambano nao.

Na ni lazima yachukuliwe maisha ya Mtume (saw) akiwa Makkah kuwa kiigizo cha kufuatwa kwa mujibu wake katika ulinganizi. Itaanza katika hatua ya kusoma na kufahamu pamoja na kutenda yanayo lazimishwa na Uislamu kama ilivyokuwa hali katika nyumba ya Arqam, kisha watagura waliousoma na kuufahamu Uislamu, na kuamini kwa *ikhlas* kwa kuingiliana na Ummah mpaka waufahamu Uislamu na wafahamu dharura ya kuwepo serikali ya Kiislamu. Na ni juu ya kundi kuanza kuhutubia kwa kutaja ufisadi wao na kuwaibisha, na kupambana na fahamu zao zilizo changanyikiwa na rai zao zilizofisidika. Na kuwabainishia uhakika wa Uislamu na kiini cha ulinganizi wake mpaka iwepo kwao wote ufahamu wa busara jumla (*wai' 'amma*) juu ya ulinganizi. Walinganizi watakiwa kuwa ni sehemu ya Ummah, na utakuwa Ummah pamoja nao kwa jumla bila kugawanyika, na utafanya kazi Ummah kwa ujumla wake kazi iliyo na natija chini ya uongozi wa kundi la ulinganizi, mpaka wafikie katika utawala na waiunde serikali ya Kiislamu. Na wakati huo yatachukuliwa maisha ya Mtume (saw) akiwa Madina kama kiigizo cha kufuatwa kwa mujibu wake katika kuutabikisha Uislamu na kubeba ulinganizi wake. Na kwa haya kundi la Kiislamu ambalo hubeba ulinganizi halina mahusiano na upande wa kivitendo, wala halijishughulishi na kitu chochote kisichokuwa ulinganizi. **Na huchukulia kutenda kitendo chochote miongoni mwa vitendo vinginevyo visivyokuwa da'wah kuwa vya kupumbaza**, **kupotosha na kikwazo kwa ulinganizi wala haijuzu kata kata kujishughulisha navyo**. Mtume (saw) alikuwa akiulingania Uislamu Makka ilhali Makka imejaa ufasiki na uovu wala hakutenda kitendo chochote cha kuziondoa. Zilikuweko dhuluma, unyanyasaji na ufukara wala haikupokelewa kutokamana naye kama ametenda kitendo ili kukhafifisha vitu hivyo. Aliswali katika Ka'abah na kulikuwa na masanamu yanayopita kimo chake na wala haikupokelewa kutokamana naye kama aligusa sanamu lolote katika yale. Bali alichokifanya ni kuaibisha miungu yao, kuifanya duni fikra zao, akifichua vitendo vyao vya makosa na kujifunga na upande wa kimatamshi na kifikra Lakini pindi alipokuwa na serikali na akaikomboa Makka hakubakisha chochote katika masanamu hayo, wala ufasiki na uovu huo, wala dhuluma na unyanyasaji, wala ufukara na umasikini.

Na kwa hivyo **haijuzu kwa kundi ikiwa linabeba ulinganizi kutenda kama kundi kitendo chochote miongoni mwa vitendo vyenginevyo, na ni lazima libakie tu kwa fikra na ulinganizi isipokuwa watu hawazuiliwi kutenda wanayoyataka miongoni mwa vitendo vya msaada** lakini kundi halitendi hayo kwa sababu kazi yake ni kusimamisha serikali itakayo beba ulinganizi.

Pamoja na kuwa ni lazima kuchukuliwa maisha ya Mtume (saw) akiwa Makka kama kiigizo cha kufuata kwa mujibu wake, **yapasa kutambuliwa tofauti baina ya watu wa Makka na kulinganiwa kwao kwa Uislamu na baina ya Waislamu leo na kulinganiwa kwao kurudisha maisha ya Kiislamu**. Nayo ni kuwa Mtume (saw) alikuwa akiwalingania Makafiri kuingia katika Uislamu na amma ulinganizi leo ni kuwalingania Waislamu ili waufahamu na watende kwa mujibu wa unavyotaka.

Kwa hayo imekuwa ni lazima kwa kundi lisijichukulie nafsi yake kuwa tofauti na Ummah ambayo huishi pamoja nayo, bali kujichukulia nafsi yake kama sehemu ya Ummah huo kwa sababu Ummah ni Waislamu kama wao. Na wao sio bora kuliko yeyote miongoni mwa Waislamu hata kama wameufahamu Uislamu na kuufanyia kazi. Isipokuwa wao wamebeba mzigo mkubwa kuliko Waislamu, na walishikilia na kufuata zaidi mas'uliya ya kuwatumikia Waislamu mbele ya Mwenyezi Mungu na kufanyia kazi Uislamu. Na ni juu ya wanaharakati wa kundi la Kiislamu kujua kuwa hawana thamani jinsi watakavyo kuwa wengi idadi yao bila ya Ummah ambao wanafanyia kazi ndani yake. Kwa hivyo imekuwa jukumu lao ni kuingiliana pamoja na Ummah na kutembea pamoja nao katika mapambano na kuwatia hisia kuwa Ummah ndiyo unaofanya kazi. Na ni lazima kwa kundi kujiweka mbali na kila kitendo au kauli au ishara itakayo onyesha utengamano wake na Ummah kwa kitu chochote kiwe kidogo au kikubwa kwa sababu hili hutenganisha Ummah na ulinganizi wake na kufanya kundi kuwa ni tatizo lililo ongezwa juu ya matatizo ya mujtama ambalo hicho ni kikwazo kinachozuia mwamko wake. Ummah ni jumla usiogawanyika, na kundi husimama ili kusimamisha serikali na itabakia kuwa ni mlinzi wa Uislamu katika Ummah na serikali na ikiona katika Ummah mgeuko (kutoka haki) itautanabahisha na imani yake na uhodari wake. Na itakapoona serikali yaenda kombo itashirikiana pamoja na Ummah ili kuinyoosha kwa yale yaliyo faradhishwa na Uislamu. Kwa hivyo ulinganizi wa Kiislamu unaobebwa na kundi utafaulu na kuendelea katika njia yake ya kikawaida na ya kipekee.

Lengo la kundi ni kurudisha maisha ya Kiislamu katika biladi za Kiislamu na kubeba ulinganizi wa Kiislamu kwa ulimwengu, na njia yake ya kufikia hayo ni utawala. Na katika njia yake ya kufikia utawala ni kuusoma Uislamu na kuufahamu na kuwajenga watu kwa thaqafa itakayo leta athari katika kuleta aqliyyah (akili) ya Kiislamu na nafsiya (hisia) ya Kiislamu ili kujenga shakhsiya ya Kiislamu. Hivyo hivyo huingiliana na Ummah ili kuufahamisha Uislamu na kuufahamisha uhakika wa maslahi yake (maslahi ya Ummah) na kuwaonyesha kwamba Uislamu umeyasuluhisha (maslahi) haya na kudhamini kuyafikia kwake na kutabanni maslahi ya Ummah. Na yaendeshwe maingiliano na mapambano katika njia ya ulinganizi pamoja na mafundisho kwa wakati mmoja. Kazi hii ya kichama ni kazi ya kisiasa, kwa hivyo hapana budi uwe upande uliowazi wa kundi hili ni upande wa kisiasa kwa sababu

ndiyo njia ya kivitendo ya mwanzo ambayo huanza ndani yake ulinganizi kwa Uislamu. Na hii haimaanishi kuwa ni ulinganizi kwa siasa tu au kwa utawala tu, bali humaanisha ulinganizi kwa Uislamu na mapambano ya kisiasa ili kufikia nguvu za kusimamisha serikali ambayo itatabikisha Uislamu na kubeba ulinganizi wake. Kwa hivyo huwa ni lazima kundi litakalobeba ulinganizi wa Kiislamu kuwa kundi la kisiasa wala haijuzu liwe ni kundi la kiroho, wala kundi la kiakhlaqi, wala kundi la kielimu wala kundi la kuelimisha wala kitu chochote kati ya hayo na yanayo fanana nayo.

***Hizb ut-Tahrir*** ni chama cha Kiislamu na chama cha kisiasa kinacho jishughulisha na siasa na kinacho fanya kazi ili kuwajenga Ummah na thaqafa ya Kiislamu, na hudhihirika ndani yake upande wa kisiasa. Hizb huyakemea yanayo fanywa na wakoloni na vibaraka wao kwa kuwazuia wanafunzi na wafanyi kazi na siasa na kujaribu kuwaweka watu jumla mbali nayo. Hizb huona kama ni lazima watu wajue siasa na idhihirike kwao malezi ya kisiasa. Sio katika kazi ya kisiasa kuwabainishia watu kuwa Uislamu hujumuisha siasa wala kuwa misingi ya kisiasa katika Uislamu ni hivi na hivi, bali siasa ni kuchunga maslahi ya Ummah mzima kindani na kinje na kuendesha maslahi haya kwa msingi wa Kiislamu pekee. Haya hutekelezwa na serikali na Ummah ikiihisabu serikali juu yake. Kuyafikia haya kivitendo chama lazima kitekeleze majukumu hayo katika upande wa Ummah na utawala. Kwa hivyo Hizb ut tahrir hubeba ulinganizi wa Kiislamu ulinganizi jumla na kubainisha kwa Ummah hukmu za kiShari'ah ambazo hutatua matatizo ya kimaisha. Na chama hufanya kazi ili Uislamu uhukumu pekee na kupambana na makafiri wakoloni kung’oa mizizi ya athari yake. Vile vile hupambana na vibaraka vya wakoloni, sawa sawa wawe wale wanaobeba fikra kiongozi na mfumo wake na wanaobeba siasa zake na fikra zake.

Kubeba ulinganizi wa Kiislamu na mapambano ya kisiasa katika njia yake huwa ni katika mujtama ambao chama imekilenga kama majaal yake. Na Hizb ut-Tahrir huuchukua mujtama wa Kiislamu ulimwenguni kote ni mujtama mmoja kwa sababu suala lake lote ni suala moja nalo ni suala la Uislamu. Lakini imefanya nukta ya kianzio kuwa ni biladi za kiarabu kwa sifa yake kama sehemu ya biladi ya Kiislamu, na huchukulia kwamba kusimama kwa serikali ya Kiislamu katika biladi ya kiarabu kama kiini cha serikali ya Kiislamu ni hatua ya kawaida katika hayo.

Na mujtama katika ulimwengu wa Kiislamu uko katika mustawa mbaya wa kisiasa nao kwa jumla wake umekoloniwa na serikali za kimagharibi, na umebakia katika ukoloni hata kama baadhi ya biladi zinasherehekea utajiri mkubwa katika ulimwengu wa Kiislamu. Nao umenyenyekea kwa uongozi wa kifikra wa kirasilimali wa kidemokrasia unyenyekevu kamili na kutabikishwa juu yake katika utawala na siasa kwa nidhamu ya kidemokrasia. Na katika uchumi kwa nidhamu ya kirasilimali, nao katika upande wa kijeshi

unaoongozwa na wageni katika silaha zake, mazoezi yake na fani zilizo salia za kijeshi, na katika siasa ya kigeni inafuata siasa za kigeni za mwenye kuikoloni. Kwa hivyo twaweza kusema kuwa biladi za Kiislamu bado zimebakia katika ukoloni na bado ukoloni umekita ndani yake, kwa sababu ukoloni ni kulazimisha jeshi, siasa, uchumi, na thaqafa juu ya watu dhaifu ili kuwanyonya, nayo hutumia nguvu zote ili kulazimisha uongozi wake wa kifikra na kumakinisha mtazamo wake maishani. Na sampuli za ukoloni tofauti tofauti inajumuisha kuunganishwa kwa nchi zilizo koloniwa kwa ardhi ya nchi inayo koloni na kuanzisha koloni, na kusimamishwa kwa serikali huru kijina lakini kivitendo zinanyenyekea kwa serikali iliyo zikoloni. Huu ndiyo uhakika (waqi'ah) katika biladi za Kiislamu, uhakika wake ni kuwa zote zinanyenyekea kwa utawala wa kimagharibi na hupelekwa kwa mujibu wa mpango wa kikoloni wa kimagharibi katika upande wa kithiqafa na mawazo. Na pamoja na kunyenyekea kwake kwa utawala wa kimagharibi, zimekuwa hivyo hivyo ni lengo la uvamizi wa umoja wa kisovieti wa zamani pindi ilipokuwa ikifanya kazi ndani yake (biladi za Kiislamu) kwa kupitia vibaraka wake ili watu wauamini ukomunisti, na ili utawale uongozi wake wa kifikra na mtazamo wake maishani kwa kulingania mfumo wa kikomunisti.

Kwa hayo, zimekuwa biladi za Kiislamu ni koloni za serikali za kimagharibi na uwanja kwa uongozi za kifikra za kigeni. Hivyo hivyo zilikuwa ni kituo cha macho ya umoja wa kisovieti wa zamani na lengo la uvamizi wake na kuteka kwake si kwa ajili ya kuzikoloni. Bali kuzibadilisha biladi za Kiislamu kuwa biladi ya kikomunisti na kuibadilisha mujtama wote uwe ni mujtama wa kikomunisti utakao futwa ndani yake athari ya Uislamu. Isipokuwa kwa kuanguka kwa umoja wa kisovieti yamepotea yote hayo hata kama wamebakia baadhi wanao jinasibisha na vyama ya kikomunisti katika biladi za Kiislamu bila ya kuwa na uweza wowote wa kuathiri. Ni lazima kutekelezwa kazi ya kisiasa ili ipambane na ukoloni, na ipigane na uongozi za kifikra za kigeni na kufanya kazi ili kujikinga na hatari ya uvamizi wa kigeni ambao unalenga biladi zetu. Kubeba ulinganizi wa Kiislamu kwa njia sahihi kutapambana na hatari ya uongozi wa kifikra za kigeni. Basi ni lazima iwe kupambana na ukoloni wa kimagharibi iwe ni jiwe la msingi katika mapambano ya kisiasa.

Mapambano ya kisiasa hulazimu kutopokea misaada ya kigeni ya aina yoyote kutoka kwa mgeni pasina kujali taifa analotoka au msaada aina yoyote. Huhesabiwa kila msaada wa kisiasa kutoka kwa mgeni yeyote na kila kumlingania kwake yeye kuwa ni khiyana kwa Ummah. Na hulazimu pia kufanya kazi ili kujenga umbo (*kiyan*) la kindani katika ulimwengu wa Kiislamu mjengo mzuri ili serikali ya Kiisilamu iwe na nguvu za kiulimwengu na utawala wake wa kipekee, na mujtama wake uwe ni wa kutukuka. Na nguvu hii itafanya kazi ili ichukue nguvu za uongozi (*zimam al-mubadara*) kutoka kwa kila mwanajeshi ili ibebe ulinganizi wa Kiislamu kwa ulimwengu na

kutawalisha uongozi wake. Na pia hulazimu mapambano ya kisiasa kupigana vita na nidhamu, kanuni na sheria za kimagharibi na hali zote za ukoloni. Ni lazima kukataa mipango yote ya kimagharibi khasa ya Uingereza na Amerika, sawa sawa iwe ni mipango ya kisanii au ya kimali au ya kisiasa au aina yoyote ya mipango. Na hulazimu pia kupinga (*nabadha*) hadhara za kimagharibi, wala hilo haimaanishi kupinga aina tofauti za kimadaniyya kwa sababu madaniyya huchukuliwa ikiwa ni natija ya elimu (sayansi) na usanii. Na hulazimu pia kung'oa uongozi wa kifikra wa kigeni kutoka mizizi yake. Vivyo hivyo hulazimu pia kupinga thaqafa ya kigeni ambayo hugongana na mtazamo za kifikra wa Kiislamu. Hilo haimaanishi (kupinga) elimu (sayansi) kwa sababu elimu ni ya kiulimwengu na ni wajibu kuchukuliwa kutoka upande wowote ule kwa sababu elimu ni katika sababu muhimu ya utangulizi wa kimada maishani.

Na mapambano ya kisiasa hulazimisha tujue kuwa wakoloni wa kimagharibi khasa Uingereza na Amerika hufanya kazi katika kila biladi koloni kusaidia vibaraka wao, pamoja na wakiwemo watu walioregelea nyuma (*raji'iyin*) walio ndani ya giza, na wanaolingania kwa sera zao (za kimagharibi) na uongozi wao wa kifikra, na ikiwemo vikundi vinavyotawala. Wakoloni hawa hukimbilia kuwapa msaada vibaraka wao katika maeneo mbali mbali ili kuzuia harakati hii ya Kiislamu, na watawapa msaada wa kimali na usiokuwa wa kimali na kujumuisha nguvu zinazo lazimu ili kuimaliza (harakati hii). Na utasimama ukoloni pamoja na vibaraka wake kwa kubeba bendera ya uvumi dhidi ya harakati hii ya ukombozi wa Kiislamu kwa kuituhumu kwa tuhuma mbali mbali: '*Kama kuwa wameajiriwa na wakoloni*', *'huleta fitina ya kindani*', *'ni yenye kupelekea ulimwengu kuwageukia Waislamu"*, *"inakhalifiana na Uislamu'* na tuhuma nyinginezo zenye kufanana nazo. Kwa hivyo ni lazima wawe macho wenye kupambana na sera za kikoloni na mbinu zake mpaka wafichue njama zake za kikoloni za kindani na nje kwa wakati wake, kwa sababu kufichua njama za ukoloni kwa wakati wake huhisabiwa ni katika aina muhimu ya mapambano.

Hivyo basi, ***Hizb ut-Tahrir*** hufanya kazi ili kukomboa maeneo ya Kiislamu kutokamana na ukoloni wote na hupambana na ukoloni mapambano yasiyokuwa na mapumziko ndani yake. Lakini hailengi tu kuwafukuza kijeshi wakoloni katika biladi za Kiislamu wala uhuru wa kirongo bali hufanya kazi ili kung'oa hali ambayo zimesimamishwa na kafiri mkoloni kutoka mizizi yake kwa kukomboa biladi, taasisi na fikra kutokamana na kutawaliwa (*ihtilal*) sawa sawa iwe kutawaliwa kiaskari au kifikra au kithiqafa au kiuchumi au yasiyokuwa hayo. Hizb hupigana vita na kila anayetetea upande wowote wa kikoloni mpaka yarudishwe maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha serikali ya Kiislamu ambayo itabeba ujumbe wa Uislamu kwa ulimwengu wote. Twamuomba Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye twanyenyekea, atusaidie na

msaada kutoka Kwake ili tutekeleze majukumu haya mazito. Hakika Yeye Husikia na ni Mwenye Kujibu.

***Hizb ut-Tahrir***

***Hizb ut-Tahrir*** ni chama cha kisiasa na mfumo wake ni Uislamu. Lengo lake ni kurudisha maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha serikali ya Kiislamu itakayo tekeleza nidhamu za Kiislamu na kubeba ulinganizi wake kwa ulimwengu. Na imekwisha andaa Hizb hii thaqafa ya kichama iliyodhamini hukmu za Kiislamu katika mambo ya kimaisha. Na Hizb hulingania kwa Uislamu (kama) uongozi wa kifikra unaotokamana kwayo nidhamu ambazo hutatua matatizo yote ya mwanadamu, ya kisiasa, ya kiuchumi, ya kithaqafa, ya kijamii na mengineo yasiyokuwa hayo. Nacho ni chama cha kisiasa kinacho unganisha katika uwanachama wake wanawake kama inavyo unganisha wanaume. Na hulingania watu wote Uislamu na kutabanni ufahamu wake na nidhamu zake, na huwatizama wote vyovyote watakavyo tofautika makabila yao na madhab zao kwa mtazamo wa Kiislamu. Na hutegemea kuingiliana na Ummah ili kufikia lengo lake, na hupambana na ukoloni kwa aina zake zote na majina yake yote ili kuhakikisha kukomboa Ummah kutokamana na uongozi wake wa kifikra na kung'oa mizizi yake ya kithaqafa, kisiasa, kijeshi na kiuchumi na mengineo kutoka mchanga wa biladi za Kiislamu, na kubadilisha fahamu za makosa zilizo enezwa na mkoloni kufunga Uislamu kuwa ni ibada na akhlaqi tu.